BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

FEBRUARI, 2023

## BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

YALIYOMO


1. UTANGULIZI - 7 -
1.1 UTARATIBU NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI - 8 -
1.2 MISWADA YA SHERIA - 8 -
1.3 MUUNDO WA KAMATI - 9 -
1.4 HADIDU REJEA - 9 -
SEHEMU YA PILI - 11 -
2.1 OFISI YA RAIS – IKULU - 11 -
2.2 OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI - 12 -
2.3 OFISI YA NYARAKA - 12 -
2.4 AFISI YA USALAMA WA SERIKALI (GSO) - 14 -
3. OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA - 15 -
3.1 MAHAKAMA KUU - 16 -
3.2 AFISI YA MWANASHERIA MKUU - 18 -
3.3 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA - 19 -
Changamoto za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka Zanzibar (DPP) - 19 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa ofisi ya DPP - 20 -
3.4 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR - 20 -
Changamoto za Tume ya Kurekebisha Sheria: - 21 -
Maoni na Ushauri wa Kamati - 21 -
3.5 SKULI YA SHERIA ZANZIBAR - 22 -
3.6 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA ZANZIBAR - 23 -
3.7 OFISI YA MUFTI MKUU ZANZIBAR - 24 -
3.8 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI - 25 -
3.9 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA) - 26 -
3.10 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA - 28 -
Changamoto za Kamisheni ya Utumishi wa Umma - 28 -
3.11 AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) - 29 -
Changamoto za Afisi ya CAG Zanzibar - 30 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Afisi ya CAG Zanzibar - 30 -
3.12 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO - 31 -

Changamoto za Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar - 31 -
Maoni na Ushauri wa Kamati - 32 -
3.13 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)- 32 -
3.14 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA - 34 -
4. OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ - 35 -
4.1 JESHI LA KUJENGA UCHUMI *(JKU)* ZANZIBAR - 36 -
Changamoto za Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Zanzibar - 37 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa JKU Zanzibar - 37 -
ZIARA YA KAMATI KATIKA KAMBI YA JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT) CHITA – MOROGORO - 38 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa JKU kutokana na ziara hii - 39 -
4.2 WAKALA WA ULINZI WA JESHI LA KUJENGA UCHUMI - 39 -
Changamoto za Wakala wa Ulinzi wa JKU Zanzibar - 39 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Wakala wa Ulinzi - 40 -
4.3 CHUO CHA MAFUNZO (MF) ZANZIBAR - 40 -
Changamoto za Chuo cha Mafunzo Zanzibar - 40 -
ZIARA YA KAMATI KATIKA GEREZA LA MTEGO WA SIMBA KPF – MOROGORO - 42 -
4.4 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - 43 -
4.5 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) - 44 -
4.6 KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) - 46 -
4.7 KAMPUNI YA UJENZI YA SERIKALI....................................................-47-
4.8 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI - 48 -
4.9 BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR - 49 -
Changamoto zinazolikabili Baraza la Jiji la Zanzibar - 49 -
Maoni na Ushauri wa Kamati - 50 -
410 BARAZA LA MANISPAA MJINI - 50 -
Changamoto za Baraza la Manispaa Mjini - 51 -
Maoni na Ushauri wa Kamati - 51 -
4.11 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “A” - 51 -
Changamoto zinazolikabili Baraza la Mji Magaharibi ‘A’ - 52 -
Maoni na Ushauri wa Kamati - 52 -
4.12 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI “B” - 53 -

Maoni na Ushauri wa Kamati - 54 -
4.13 OFISI YA MKOA WA KUSINI UNGUJA - 54 -
Changamoto za Mkoa wa Kusini Unguja - 55 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mkoa wa Kusini Unguja: - 55 -
4.14 BARAZA LA MJI KATI - 56 -
Changamoto zinazowakabili Baraza la Mji Kati: - 56 -
Maoni na ushauri wa Kamati: - 57 -
4.15 HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA - 57 -
Changamoto za Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja - 58 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja - 58 -
4.16 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA - 59 -
4.17 BARAZA LA MJI KASKAZINI “A” - 59 -
Changamoto Za Baraza La Mji Kaskazini “A” Unguja - 60 -
Maoni na Ushauri wa Kamati - 60 -
4.18 BARAZA LA MJI KASKAZINI “B” - 61 -
Changamoto Za Baraza La Mji Kaskazini “B” - 61 -
Maoni na Ushauri wa Kamati - 62 -
4.19 OFISI YA MKOA WA KUSINI PEMBA - 63 -
Changamoto Zinazoukabili Mkoa wa Kusini Pemba: - 63 -
4.20 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE - 64 -
4.21 BARAZA LA MJI MKOANI – PEMBA - 66 -
4.22 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI PEMBA - 67 -
4.23 BARAZA LA MJI WETE - 68 -
Changamoto za Baraza La Mji Wete - 69 -
Maoni na ushauri wa Kamati - 69 -
4.24 HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI - 69 -
4.25 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR - 71 -
5. OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS - 73 -
6. OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI - 79 -
6.1 BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR - 80 -
Changamoto za Baraza la Wawakilishi Zanzibar - 81 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar - 81 -

6.2 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR - 81 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar - 82 -
6.3 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF) - 82 -
Changamoto za Utekelezaji wa Programu - 83 -
Maoni na Ushauri wa Kamati kwa TASAF - 84 -
7.0 MAONI NA USHAURI WA JUMLA - 85 -
Ofisi ya Rais Ikulu - 85 -
Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora - 86 -
Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - 87 -
Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - 89 -
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi - 90 -
8.0 HITIMISHO - 91 -

# SEHEMU YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambayo imeundwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa kifungu cha *85* cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* na Kanuni ya *107(1)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka *2020*.

Ripoti hii inaakisi kazi zote za Kamati ambazo zimefanywa kuhusiana na utekelezaji wa Taasisi ambazo zipo chini yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha, 2022/2023 na kwa kuzingatia Mipango mikuu ya Kitaifa ambayo inajumuisha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Ilani ya Chama Chama Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025. Aidha, majukumu ya Kamati hii, yameelezwa katika *Jadweli la Kwanza* la Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kama ifuatavyo:

(i) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.
(iii) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
(iv) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
(v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
(vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.
(vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.
(viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati hii ni ya Kisekta ambayo inasimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara *Tano (5)* zifuatazo: -

*(a)* Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.
*(b)* Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.
*(c)* Ofisi ya Makamu wa Kwanza Rais.
*(d)* Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, na
*(e)* Ofisi ya Rais Ikulu.

## 1.1 UTARATIBU NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Sehemu hii inaelezea utaratibu uliotumiwa na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika utekelezaji wa kazi zake ambazo zilifanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi

Zanzibar, Toleo la mwaka 2020. Shughuli hizo ni pamoja na:

(a) kupokea taarifa mbali mbali za kila robo mwaka (quarterly reports);
(b) kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya kila Wizara;
(c) utekelezaji wa Maagizo ya Kamati;
(d) kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati;
(e) kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali ya kimaendeleo inayosimamiwa na Wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa, changamoto zilizopo na kutoa ushauri wa kutatua changamoto hizo; na
(f) kupitia Miswada mbali mbali ya sheria ambayo iliwasilishwa mbele ya Kamati katika kipindi chote hicho.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa kusimamia malengo yafuatayo:

*(a)* kufuatilia maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka *2021/2022*;
*(b)* kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka wa fedha *2022/2023*;
*(c)* kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka wa fedha *2022/2023*; na
*(d)* kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika Taasisi za Serikali pamoja na kufanya ziara za ukaguzi katika Taasisi husika.

## 1.2 MISWADA YA SHERIA

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati hii ni kushughulikia miswada ya sheria ambayo itahitaji kufanyiwa mapitio na kujadiliwa katika Baraza la Wawakilishi ili kuwa sheria kamili. Katika kipindi hiki, Kamati ilipitia Miswada ifuatayo:

*(a)* Mswada wa Kufuta Sheria ya Baraza la Wawakilishi (Kinga, Uwezo na Fursa), Nam. 4 ya 2007;

*(b)* Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa), Nam. 9 ya 2006;

*(c)* Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma, Nam. 1 ya 2007 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo;

*(d)* Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake, 2022;

*(e)* Ripoti ya Tume ya Maadili kwa mwaka 2021/2022.

## 1.3 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaundwa na Wajumbe wafuatao:

| ***Nam.*** | ***Jina*** | ***Wadhifa*** |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg.Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama. |

## 1.4 HADIDU REJEA

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika kutekeleza majukumu yake ilitumia:

*(a)* Katiba ya Zanzibar ya Mwaka *1984*;
*(b)* Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka *2020*;
*(c)* Ripoti ya Kamati ya Mwaka 2022/2023;
*(d)* Hotuba za Bajeti kwa Mwaka wa fedha *2021/*2022 na *2022/2023* za Wizara zifuatazo:
  *(i)* Ofisi ya Rais Ikulu,
  *(ii)* Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora;
  *(iii)* Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ;
  *(iv)* Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;
  *(v)* Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;
*(e)* Taarifa za Utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi husika.

## SEHEMU YA PILI

## 2. MAUDHUI YA RIPOTI YA KAMATI

Sehemu hii inaelezea kwa kina mafanikio, changamoto na ushauri wa Kamati kwa kila taasisi ambayo ipo chini ya usimamizi wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kipindi cha mwaka 2022/2023. Taasisi hizo ni:

(a) Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora;
(b) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ;
(c) Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;
(d) Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; na
(e) Afisi ya Rais Ikulu.

### 2.1 OFISI YA RAIS – IKULU

Afisi ya Rais – Ikulu inatekeleza na kusimamia programu kuu sita ambazo ndani yake zimo programu ndogo ndogo, kumi na tatu zenye kuakisi mipango yote ya Afisi kwa upande wa Unguja na Pemba. Katika utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za mandeleo, Kamati imefanikiwa kutembelea na kukagua shughuli mbali mbali ambazo zimepangwa kutekelezwa kwa kipindi hiki cha utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023.

Aidha, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa programu zote zilizopangwa na kwa namna zilivyotekelezwa kwa wakati na kwa ufanisi wa hali ya juu.

Katika programu kuu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi; Kamati inaishauri Afisi kuzidisha kasi ya kuwafikia walengwa na kuangalia maendeleo yao kama Wazanzibari wengine pamoja na kuimarisha uhusiano wa kikanda kwa kushiriki vikao na makongamano mbali mbali ambayo yanafanywa na nchi wananchama.

## 2.2 OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ina jukumu la kuratibu mambo yanayohusu Baraza la Mapinduzi pamoja na Kamati zake ikiwepo Kamati ya Makatibu Wakuu *(Inter Ministerial Technical Committee - IMTC)*.

Ofisi hii inatekeleza majukumu yafuatayo:

*(a)* Kuandaa mikutano ya Baraza la Mapinduzi na kutunza taarifa za mikutano.
*(b)* Kuchambua nyaraka zitazowasilishwa Baraza la Mapinduzi na Kamati zake.
*(c)* Kuwasilisha maamuzi na maelekezo kwa taasisi za utumishi wa umma zinazohusika.
*(d)* Kutoa msaada wa kufanya utafiti kwa Baraza la Mapinduzi katika mambo yanayongoja au yanayotarajiwa kuwasilishwa katika Baraza hili.
*(e)* Kutekeleza majukumu mengine yoyote kama Katibu Mkuu Kiongozi atakavyoona inafaa ikiwemo kuendesha programu za kujenga uwezo kwa viongozi wa ngazi za juu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kamati imeridhishwa na kazi zinazofanywa na Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa kuzingatia mustakabali mzuri wa nchi yetu.

## 2.3 OFISI YA NYARAKA

Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Zanzibar imeundwa na kufanya kazi chini ya Sheria Nam. 3 ya Mwaka 2008 ambapo imepewa majukumu ya msingi katika kutunza na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu kama urithi wa Taifa.

Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar imefanikiwa kuzihuisha nyaraka ishirini na tano, kufanya ukaguzi na kutoa ushauri na maelekezo juu ya usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka kwa wasimamizi wa kumbukumbu na nyaraka katika wizara, idara, mashirika na taasisi za umma ili kuzihifadhi katika njia ambazo zitakuwa salama kwa matumizi ya sasa na baadae.

Aidha, Ofisi imeingia mkataba wa mashirikiano na Taasisi ya Chuo Kikuu cha Norway (Bergen University) katika utambuzi wa nyaraka zilizoandikwa kwa mkono (Islamic Manuscripts) zinazohusiana na historia ya Dini ya Kiislamu kwa jamii ya Zanzibar.

### Changamoto za Taasisi ya Nyaraka Zanzibar

Licha mafanikio kadhaa ambayo yamepatikana katika kipindi hiki, Kamati imeweza kubaini changamoto ndogo ndogo ambazo kimsingi zinahitaji utatuzi kama ifuatavyo:

*(a)* ufinyu wa Ofisi kwa watendaji na sehemu ya kuhifadhia nyaraka zinazokusanywa na zilizopo;
*(b)* ukosefu wa mfumo bora wa kupoza hewa katika chumba cha kuhifadhia nyaraka (strong room);
*(c)* taasisi nyingi zilizopewa miongozo na mafunzo muhimu ya utunzaji kumbukumbu na nyaraka zinaonekana kutotilia maanani na kutoyatekeleza kivitendo mafunzo na miongozo waliyopewa;
*(d)* kutopewa umuhimu na kipaumbele kwa ripoti za ukaguzi zinazowasilishwa kwa wakuu wa taasisi za Serikali;
*(e)* kupotea na kuharibika kwa wingi wa kumbukumbu na nyaraka muhimu zinazozalishwa na kuhifadhiwa katika baadhi ya Taasisi na idara zake, kwa mfano Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Elimu.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Taasisi ya Nyaraka Zanzibar**

*(i)* Kamati imeridhika na uongozi mpya wa taasisi hiyo lakini pia tunaishauri Serikali kujenga kwa mahusiano mazuri baina ya Taasisi hii ya Zanzibar na Taasisi ya Kumbukumbu na Nyaraka ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuongeza ujuzi kwa kujifunza kwa vitendo juu ya namna bora ya uhifadhi wa nyaraka kila inapohitajika;
*(ii)* Kamati inaishauri Taasisi kukamilisha kwa haraka mpango wake wa marekebisho ya sheria, muundo wa Taasisi, Sera na Kanuni za Taasisi;
*(iii)* Taasisi ipatiwe jengo la kisasa lenye uwezo wa kuhifadhia kumbukumbu tuli;
*(iv)* Taasisi izidishe mashirikiano na taasisi za umma na binafsi kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kuhifadhia kumbukumbu na kutunza historia ya Zanzibar;
*(v)* kuwajengea uwezo watendaji wake kwa lengo kuwa na wataalamu wa kutosha katika sekta hii pamoja na kuondosha changamoto za kitaalamu;
*(vi)* kuendeleza mpango wa ujenzi wa jengo jipya katika eneo la Kilimani kwa kufuatilia na kununua nyumba zilizopo katika eneo hilo.

## 2.4 AFISI YA USALAMA WA SERIKALI (GSO)

Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO) inafanya kazi chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya mwaka 2011, kifungu 78(1), (2), (3), (4) na (5) na Utaratibu wa Utendaji kazi wa GSO wa mwaka 1994 uliotolewa na Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

Afisi ya Usalama wa Serikali Zanzibar imefanikiwa kwa kiasi kikubwa

kutekeleza majukumu yake makuu ambayo ni:

(i) kufanya Upekuzi wa Kiusalama,
(ii) kufanya Ukaguzi wa majengo ya makaazi ya Viongozi Wakuu wa Serikali, majengo ya Afisi za Serikali na miundombinu ya Serikali,
(iii) kutoa Mafunzo ya kiusalama yanayohusu utunzaji wa siri na nyaraka za Serikali ikiwemo na kusimamia kiapo cha utunzaji wa siri katika Wizara, Idara, Mashirika ya Serikali ili kuwafanya watumishi wote wa Serikali na Mashirika yake kuwa na mwamko na uelewa wa majukumu yao ya kiusalama,
(iv) Afisi imefanikiwa kutoa Mafunzo ya Usalama kwa Watumishi wa Umma kuhusu Sheria na Kanuni zinazotawala Udhibiti wa Siri na Nyaraka za Serikali na Usalama wa Serikali kwa jumla ambapo jumla ya wafanyakazi mia mbili na kumi na mbili (212) wamepatiwa mafunzo hayo na jumla ya majengo saba (7) yamefanyiwa ukaguzi.

**Changamoto zinazoikabili Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO) Zanzibar**

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Afisi ya GSO inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* kuchelewa na uchache wa fedha za matumizi ya kawaida (OC) jambo linalopelekea kuchelewa kwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa hasa kwa maeneo yalioko nje ya Unguja kama vile Pemba na Dar es salaam;
*(ii)* kukosekana kwa mrejesho wa mapendekezo yanayotolewa na Afisi ya Usalama wa Serikali baada ukaguzi wa kiusalama wa majengo;
*(iii)* kutokutekelezwa kwa vitendo Miongozo na mafunzo ya Utunzaji na Udhibiti wa Siri za Serikali yanayotolewa na GSO katika utendaji wao wa kazi wa kila siku na baadhi ya taasisi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Afisi ya Usalama wa Serikali (GSO) Zanzibar**

*(a)* Kamati inaishauri Afisi hii kuzidisha kasi ya kutoa mafunzo ya kiusalama kwa watendaji juu ya umuhimu wa kuhifadhi siri za Serikali na nyaraka za nchi yetu kwa ujumla;
*(b)* Kamati pia, inashauri Afisi kufanya ukaguzi katika majengo ya umma na yale ya kibishara kwa lengo la kuiweka nchi yetu katika hali ya kiusalama;
*(c)* Kamati inaitaka Afisi kufanya ukaguzi wa kiusalama katika eneo la kuhifadhia mafuta la Wesha, kwani imeona hali ya matangi katika eneo hili si salama kwa wakaazi na watumiaji wa Bandari ya Wesha Pemba;
*(d)* Kamati imesikitishwa kuona zipo baadhi ya taasisi ambazo hazitekelezi kwa vitendo Miongozo na mafunzo ya Utunzaji na Udhibiti wa Siri za Serikali

yanayotolewa na GSO katika utendaji wao wa kazi wa kila siku. Hivyo, Kamati inazitaka taasisi husika kuwachukulia hatua watumishi wote wanaokaidi miongozo hiyo kwa vitendo.

## 3. OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia masuala ya Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Ofisi hii ina jumla ya Idara na Taasisi 11 zinazosimamiwa na Katibu Mkuu na Taasisi 01 inayopokea Ruzuku kutoka Serikalini. Idara na Taasisi hizo ni kama zifuatavyo:

*(a)* Idara ya Utumishi na Uendeshaji,

*(b)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,

*(c)* Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi,

*(d)* Wakala wa Serikali Mtandao,

*(e)* Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma,

*(f)* Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu,

*(g)* Idara ya Msaada wa Kisheria,

*(h)* Idara ya Utawala Bora,

*(i)* Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar,

*(j)* Ofisi ya Waqfu na Mali ya Amana,

*(k)* Afisi Kuu Pemba.

Aidha, Chuo cha Utumishi wa Umma *(IPA)* kinapokea ruzuku kutoka Serikalini ili kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Vile vile, Wizara hii inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:

*(a)* Mahkama Kuu,

*(b)* Afisi ya Mwanasheria Mkuu (AGC),

*(c)* Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP),

*(d)* Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

*(e)* Tume ya Kurekebisha Sheria,

*(f)* Kamisheni ya Utumishi wa Umma,

*(g)* Tume ya Utumishi Serikalini,

*(h)* Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA).

Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imegawika katika sekta kuu tatu (3) ambazo ni Sekta ya Sheria, Sekta ya Uratibu wa Utumishi wa Umma na Sekta ya Utawala Bora.

*Sekta ya Sheria* inahusisha Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa haki, Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria, Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai, Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria na Programu ya Usimamizi wa Masuala ya dini. Programu hizi zinatekelezwa kupitia Mahkama Kuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria, Ofisi ya Mufti, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Idara ya Msaada wa Kisheria.

## 3.1 MAHAKAMA KUU

Mahakama Kuu Zanzibar ina jukumu la kutafsiri sheria, kusikiliza kesi na kutoa uamuzi kufuatana na sheria za nchi. Vile vile, Mahakama ina jukumu la kusikiliza na kutoa uamuzi wa kesi zote zinazohusiana na masuala ya jinai na madai.

Kamati imeridhishwa na utendaji wa Mahakama ikiwemo Mahakama ya Kadhi Zanzibar kwa juhudi zao za kutetea haki na kuijenga jamii yenye maadili mema. Hata hivyo, katika kipindi kifupi cha julai – Septemba, 2022, Mahakama ya Kadhi imefanikiwa kupokea mashauri 597 na kuyatolea maamuzi mashauri 538. Aidha, mashauri 414 ya Talaka yalifunguliwa na kutolewa maamuzi mashauri 316 kwa kufuata misingi ya Dini ya Kiislamu.

Katika kipindi hiki Kamati imebaini kwamba Mahakama imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:

*(i)* kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi mbali mbali za jinai na madai kulingana na wakati husika;

*(ii)* kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi zote za udhalilishaji ambazo zilifunguliwa katika Mahakama mbali mbali Unguja na Pemba;

*(iii)* kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu haki za watendaji wa Mahakama, waheshimiwa Mahakimu na Majaji wa Mahakama Kuu;

*(iv)* kuanzisha mfumo maalumu wa kielektroniki wa kuhifadhia mashauri ambao utaenda kupunguza changamoto ya mrundikano wa kesi katika Mahakama mbali mbali.

### Changamoto za Mahkama Zanzibar

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Mahkama inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(a)* kuwepo kwa uchakavu mkubwa wa majengo ya Mahakama ambao umedumu kwa muda mrefu sasa hasa katika Mahakma za Wete, Mkoani, Konde na Mkokotoni;

*(b)* Kamati imebaini kwamba katika taratibu za kisheria Zanzibar inaruhusika Mahkama kutoa adhabu ya kuitumikia jamii kwa wahalifu lakini bado mpaka leo sheria hii haijatekelezwa na hivyo kusababisha mrundikano mkubwa wa mahabusu na wanafunzi katika Chuo cha Mafunzo ambapo kunaipa mzigo mkubwa Serikali katika kuwahudumia wanafunzi ambao wengine wanakabiliwa na kesi ndogo ndogo;

*(c)* uhaba wa fedha za matumizi mengineyo ambapo uingiaji wa fedha hizo haukidhi mahitaji ya Mahakama;

*(d)* uchakavu na ukosefu wa vyombo vya usafari kwa watumishi wa Mahakama za Mikoa;

*(e)* ukosefu wa gari la Mheshimiwa Kadhi Mkuu wa Zanzibar anapokuwa kisiwani Pemba;

*(f)* ukosefu wa majengo ya ofisi za Mahkama ya Kadhi Unguja na Pemba;

*(g)* kuwepo kwa changamoto ya ulinzi wakati wa kuendesha kesi katika Mahkama za Kadhi hususan Mahkama ya Mwanakwerekwe sehemu ambayo hupokea kesi nyingi zaidi kuliko Mahkama zote za Zanzibar na hivyo kupelekea baadhi ya kesi kuwa na migogoro mipya baada ya kutolewa hukumu;

*(h)* Kamati pia imebaini kuwepo kwa kituo cha Usuluhishi wa kesi za ndoa katika Mahkama ya Mwanakwerekwe ambapo kituo hiki hakitumiki kwa muda mrefu sasa tokea kuzinduliwa kwake mwaka 2018.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mahakama**

*(a)* Kamati inazishauri Mahakama ziendelee kufanya matengenezo ya majengo yake ya Mikoa ili kutanua wigo wa watendaji kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi;

*(b)* Kamati inatoa ushauri kwa wananchi kuzitumia Mahakama zilizo karibu nao badala ya watu wote kukimbilia Mahkama ya Mwanakwerekwe na hivyo kuongeza msongomano wa watu;

*(c)* Kamati inaishauri Mahakama kuweka utaratibu maalum wa kupeleka gari ya Mheshimiwa Jaji Mkuu Kisiwani Pemba;

*(d)* Kamati inaishauri Serikali kuzisaidia Mahakma hususan Mahkama ya Kadhi kupatiwa vyombo vya usafiri ili kuwasaidia katika kutekeleza shuhguli zao;

*(e)* Aidha, Kamati inashauri Mahkama ya Kadhi nayo kupatiwa ulinzi wa kutosha wakati wa uendeshaji wa kesi kwani kufanya hivyo kutawajengea imani Mahakamu wetu wakati wa kutoa hukumu za kesi katika Mahkama hizi;

*(f)* Vile vile, Kamati inaishauri Mahkama kuifanyia matengenezo nyumba Mheshimiwa Jaji Mkaazi Kisiwani Pemba pamoja na kupatiwa samani (furniture) mpya na zenye uhakika wa matumizi.

## 3.2 AFISI YA MWANASHERIA MKUU

Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 ndio Mshauri Mkuu wa Serikali kwa mambo yote ya Kisheria.

Kamati imeridhishwa na utendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa jitahada zake za kusimamia na kuendeleza majukumu yake ya  na shughuli mbalimbali za kisheria ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, Uandishi wa Miswada ya Sheria, Kusimamia Kesi na Mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali, Kuandaa Hati za Nyaraka za Kisheria, Kusimamia Mikataba yote ambayo Serikali ni sehemu ya Mikataba hiyo na kufanya mambo mengine ya Kisheria kwa niaba ya Serikali.

**Changamoto zinazoikabili Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar**

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(a)* Ucheleweshaji wa taarifa zinazoombwa na Afisi kutoka taasisi zinazolalamikiwa hali inayopelekea uchelewaji wa kutoa majibu kwa walalamikaji.

*(b)* Kukosekana kwa usafiri wa Gari Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba ambao kwa sasa wanatumia honda hali ambayo sio salama kwa mawakili wanapokwenda Mahakamani.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu**

*(a)* Kamati inaziomba Taasisi ambazo zinalalamikiwa kuharakisha majibu ya walalamikaji ili kuwarahisishia Afisi ya Mwanasheria kumaliza mashauri yao kwa wakati.

*(b)* Kamati inashauri Afisi ya Mwanasheria kuliangalia suala la usafiri kwa upande wa Pemba ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

## 3.3 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar ndio yenye dhamana ya kuendesha kesi za jinai hapa Zanzibar kwa kufuata utaratibu uliowekwa kisheria. Katika utekelezaji wa majukujmu yake Afisi hii imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuendesha kesi zake kwa wakati na kuzisimamia ipasavyo ili kuona haki inatendeka kwa mujibu wa sheria.

Sambamba na hayo, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutokana na mashirikiano yaliyojengeka kupitia taasisi za haki jinai baada ya kuondoka kwa mgogoro wa muda mrefu uliokuwepo baina ya taasisi hizo na kukwamisha ufanisi wa uendeshaji wa kesi.

**Changamoto za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka Zanzibar (DPP)**

Pamoja na kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Afisi ya DPP inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(a)* ukosefu wa majengo ya Afisi za Mwendesha Mashtaka kwa upande wa Pemba;

*(b)* kuwepo na ukosefu wa madarasa ya kufundishia kwa Kituo cha Utafiti wa Skuli ya Sheria Zanzibar;

*(c)* ukosefu wa vyombo vya usafiri;

*(d)* wananchi wengi kushindwa kufika Mahkamani kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji;

*(e)* wananchi kutumia mwanya wa kesi za udhalilishaji kubambikizana kesi za uongo, jambo ambalo linarudisha nyuma mapambano dhidi ya utafutaji wa haki katika jamii;

*(f)* uhaba wa watendaji kwa baadhi ya Afisi za Mikoa na hivyo kupelekea baadhi ya kesi kutoshughulikiwa kwa wakati.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa ofisi ya DPP**

*(a)* Kamati inaishauri Afisi ya DPP kuongeza bidii ya kuwasomesha watendaji wake kwa lengo kupata wataalamu zaidi wa kusimamia na kuendesha kesi;

*(b)* Afisi ifanye mpango wa kukitangaza Chuo cha Utafiti wa Sheria Zanzibar ili kuongeza wanafunzi kutoka sehemu mbali mbali nje ya Zanzibar;

*(c)* Kamati inaishauri Afisi kutumia mbinu mbadala ya kuwatumia Masheha na viongozi wa Dini kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kufika Mahkamani na kutoa ushahidi;

*(d)* Kamati pia inaishauri Afisi kufuatilia kwa ukaribu changamoto ya usafiri na kulipatia ufumbuzi kwa kadri hali inavyoruhusu;

*(e)* Kamati inaiomba Serikali kuangalia kwa umuhimu wake suala la wananchi kubambikiziana kesi za udhalilishaji bila ya kuwepo ukweli wake au kwa lengo tu la kuchafuana;

*(f)* Kamati inashauri ofisi hii kuwachukulia hatua wale wote wenye kupeleka kesi za udhalilishaji kwa kupanga au kukusudia kuchafuana katika jamii.

## 3.4 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imeanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria Namba 16 ya Mwaka 1986. Katika utekelezaji wa mpango wa bajeti sambamba na majukumu ya Tume hii, Kamati imeridhishwa na utendaji wake kutokana na mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika kipindi hiki kifupi.

Aidha, Tume imefanikiwa kuzipitia na kuzifanyia marekebisho sheria mbali mbali ambazo ziliagizwa kufanyiwa mapitio kwa mwaka uliopita lakini pia kuishauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuziandika upya sheria ambazo zimekuwa na muda mrefu ikiwemo sheria ya Fidia ya Mwaka 1986.

**Changamoto za Tume ya Kurekebisha Sheria:**

Palipo na mafanikio hapakosi changamoto hivyo Tume ya Kurekebisha Sheria inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(a)* Uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya sheria pamoja na kutokufahamika kwa Tume ya Kurekebisha Sheria na majukumu yake katika jamii;

*(b)* Kuwepo kwa sheria nyingi zenye mapungufu na zinazohitaji kufanyiwa marekebisho;

*(c)* Kutokuwepo mazingira bora ya kufanyia kazi kunakosababishwa na uchakavu wa jengo, ufinyu wa nafasi ya ofisi na uhaba wa vyombo vya usafiri;

*(d)* Uhaba wa fedha za matumizi kwa mujibu wa bajeti iliyowasilishwa.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

(a) Kamati inaishauri Serikali kuipatia Tume jengo la kisasa ambalo litakidhi haja kwa wafanyakazi wake;

(b) Kamati inashauri Tume kuzifanyia mapitio sheria zote zenye kuleta ugumu wa utekelezaji wake kila inapoona inafaa kufanya hivyo;

(c) Kamati inazishauri taasisi za Serikali kutoa mashirikiano ya moja kwa moja na Tume ili kuzipitia sheria za taasisi zao kwa ufanisi Zaidi;

(d) Kamati inaishauri Serikali kuunga mkono juhudi za Tume kwa kuwapatia fedha za kutosha za matumizi kwa wakati ili kusaidia kutoa mafunzo kwa watendaji wake na kutoa elimu kwa jamii;

(e) Kamati pia inaishauri Serikali kufanya utaratibu wa kuongeza wataalamu wa sharia kwa kuajiri au kuhamisha kutoka ofisi moja na kwenda Tume ili kuongeza nguvu katika utekelezaji wa majukumu yao.

## 3.5 SKULI YA SHERIA ZANZIBAR

Katika kukuza na kuimarisha sekta ya sheria Zanzibar, Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Skuli maalumu ya Sheria ambayo inahusika na kutoa

mafunzo na kuwajengea uzoefu wanasheria. Programu hii imefanikiwa sana kutekeleza malengo yaliyokusudiwa katika kujenga mustakbali bora wa fani ya sheria nchini.

Aidha, Skuli imefanikiwa kuendeleza udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Skuli kwa njia ya matandao (online admission system) ambapo mfumo huo utaiwezesha Skuli kutambua uhalali wa vyeti wanavyotoa na wanafunzi wanaojiunga na Skuli. Kwa mwaka huu, zoezi la udahili limeendelea vyema na wanafunzi waliofanikiwa wanaendelea na masomo yao.

**Changamoto za Skuli ya Sheria Zanzibar:**

Mbali ya kuwepo kwa mafanikio yaliyoelezwa hapo juu, Skuli ya Sheria inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Ukosefu wa majengo na madarasa ya kujifunzia;

(b) Uhaba wa vitabu vya kujifunzia katika maktaba;

(c) Uhaba wa vyombo vya usafiri;

(d) Uhaba wa wanafunzi kutoka Zanzibar katika fani mbali mbali.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Skuli ya Sheria Zanzibar**

*(a)* Kamati inaishauri Serikali kuipatia Skuli majengo yake ya kudumu ambayo yatasaidia kufikia malengo ya Skuli licha ya harakati hizi kuanza lakini bado juhudi za makusudi zinahitajika ili kufikia malengo kwa wakati;

*(b)* Skuli ifanye jitihada ya kuweka maktaba yenye vitabu vya kutosha kwa ajili ya wanafunzi ilikuwarahisishia katika masomo yao;

*(c)* Skuli ifuatilie kikamilifu suala la usafiri na kutatua changamoto hii kwa wakati;

*(d)* Skuli ijitangaze zaidi katika maeneo mengi ya nchi na maeneo ya nchi jirani ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kupata mapato zaidi.

## 3.6 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA ZANZIBAR

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar ni miongoni mwa Taasisi za kidini ambazo zinafanya kazi kwa maslahi ya waumini wa Dini ya Kiislamu Zanzibar. Katika awamu hii ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Kamisheni imekuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kukuza uchumi wa nchi tofauti na ilivyozoeleka kwa taasisi za kidini kushiriki katika masuala ya kukuza uchumi wa nchi.

Aidha, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hii kwa kipindi hiki na tumefurahishwa kuona jamii ipo pamoja na kuunga mkono juhudi za Kamisheni kutokana na kuitumia kila inapostahiki.

**Changamoto za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar**

Sambamba na mafanikio yaliyopatikana katika Ofisi hii, bado Kamisheni inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Jamii kutorithi kwa wakati au kutorithi kabisa kinyume na maamrisho ya Dini yetu ya Kiislamu ambapo hupelekea migogoro mingi ya mirathi katika jamii,

*(ii)* Uhaba na uchakavu wa vyombo vya usafiri kwa ofisi zote za Unguja na Pemba,

*(iii)* Familia nyingi kushindwa kuitumia Ofisi hii kwa lengo la kufanya mirathi kisheria na mambo mengine yanayohusiaka;

*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa watumishi wenye fani ya uchumi katika misingi ya Kiislamu,

*(v)* Mfumo wa ZAN malipo kwa Kamisheni ya Wakfu unaathiri shughuli za matumizi ya Ofisi,

*(vi)* Kutokufanyiwa marekebisho Sheria ya Kamisheni ya Wakfu kwa muda sasa ambapo mabadiliko mengi ya kiutendaji yanahitajika.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Kamisheni ya Wakfu**

*(i)* Kamisheni izidishe bidii katika kutoa elimu ya mirathi kwa jamii,

*(ii)* Kamati inaishauri Kamisheni kusimamia ipasavyo na kuweka taarifa sahihi za mashamba ya Wakfu kwa Unguja na Pemba sambamba na kuzitambuba mali zote za Wakfu ambazo kwa muda mrefu hazitumiki kisheria,

*(iii)* Kamati inaishauri Serikali kupitia Afisi ya Mwanansheria Mkuu kuwatambua wanasheria wa Kamisheni kama Mawakili wa Serikali ili kwenda sambamba na taasisi nyengine za umma ambazo zimekuwa na wanasheria wa kuzisaidia taasisi zao kusimamia haki na fursa zao. Aidha, Kamisheni inapaswa kufuatilia kwa ukaribu sula hili ambalo zaidi limeithiri ofisi ya Pemba kiutendaji,

*(iv)* Kamati inahimiza kuajiri vijana wa kutosha wakiwemo wataalamu wa mirathi na ili kuwawezesha kutoka hatua waliyosasa na kwenda hatua nyengine ya kiuzalishaji baada ya kupata wataalamu wa kiuchumi kutoka Serikalini,

*(v)* Kamati inapendekeza kwa Serikali kuangalia Kamisheni ya Wakfu kwa njia iliyo

bora ya utaratibu wa malipo ambao hautosumbua shughuli za utekelezaji wa Ofisi hiyo,

*(vi)* Kamati inaiomba Kamisheni kuharakisha marekebisho ya Sheria ili iweze kukidhi haja ya masuala yote ya mirathi na mambo mengine.

## 3.7 OFISI YA MUFTI MKUU ZANZIBAR

Dhamira kuu ya Ofisi ya Mufti ni kukuza uadilifu, ufanisi katika kutoa fatwa, utatuzi wa migogoro na kusimamia mambo muhimu ya kiislamu.

Kamati imeridhishwa na utendaji wa Taasisi hii katika kujenga amani kwa waumini wa Dini pamoja na kuhakikisha amani na utulivu wa nchi yetu imelindwa kwa misingi ya Dini. Aidha, Kamati inaipongeza Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake na kuhakikisha migogoro ya Dini imepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na hatua mbali mbali zinazochukuliwa katika kukabiliana na changamoto za waumini.

### Changamoto za Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar

Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa nafasi za kufanya kazi;

*(ii)* Uhaba wa wataalamu wa fani mbalimbali za dini ya kiislamu;

*(iii)*Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya kufuatilia kazi za ofisi;

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Ofisi ya Mufti Mkuu**:

*(i)* Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar isichoke kuchukua hatua na kutoa miongozo ya kidini wakati wote wanapoona inafaa kufanya hivyo.

*(ii)* Kamati inashauri kuharakisha suala la migogoro mbali mbali ambayo inaletwa kwao ili iweze kumalizika kwa muda mfupi.

*(iii)*Kamati inaelekeza Ofisi ya Mufti kuongeza vipindi vya kuelimisha jamii juu ya masuala mbali mbali ya dini na kupitia hutba za sala za ijumaa wanazoziandaa.

## 3.8 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Tume ya Utumishi Serikalini ni chombo kinachojitegemea kilichoanzishwa na

Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 chini ya kifungu 117, Toleo la 2010 na kifungu 33 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, nambari 2 ya mwaka 2011. Tume kwa ujumla ina jukumu la kusimamia Utumishi katika Serikali kwa uadilifu na kufuata misingi ya Utawala Bora.

Katika kipindi hiki Tume imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria pamoja na miongozo kutoka Serikalini. Sambamba na hayo, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Tume kwa kipindi hiki licha ya changamoto kadhaa ambazo zimekuwa zikiathiri sekta ya Utumishi nchini.

**Changamoto za Tume ya Utumishi Serikalini**

Kamati wakati ikifuatilia utekelezaji wa kazi zake imegundua Tume ya Utumishi Serikalini inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Uelewa mdogo wa watumishi juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake katika kuwahudumia wananchi.

*(ii)* Watumishi wengi wa Zanzibar kutofanya kazi kwa moyo wa kujitolea na hivyo kuweka mbele maslahi binafsi.

*(iii)* Taasisi nyingi za Umma zinachelewa kuwafanyia watendaji wapya mafunzo ya awali na hivyo kuchelewa kufanyiwa uthibitisho.

*(iv)* Tume kutofanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa Taasisi za Umma kunapelekea baadhi ya watendaji kujisahau na kuacha majukumu yao ya msingi.

*(v)* Kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa kutoa taarifa kwa watu wanaoomba ajira na kutopatiwa taarifa endapo wamekosa kuajiriwa kwa sababu za msingi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Tume ya Utumishi Serikalini**

*(i)* Kamati inashauri Tume kutoa elimu juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na Kanuni zake kwa watumishi wote wa sekta za umma;

*(ii)* Kamati inashauri Tume kutoa uelewa kwa watumishi juu ya mikataba ya kazi pamoja na mambo yote muhimu yanayohusiana na utumishi kama vile ardhilhali na barua ya kuthibitishwa kazi;

*(iii)* Kamati inashauri Tume kuweka utaratibu wa kuzikagua taasisi za Umma mara kwa mara ili kubaini mapungufu yanayojitokeza;

*(iv)* Tume inashauriwa kuwachukulia hatua watumishi wenye kutekeleza majukumu yao kinyume na Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma; na

*(v)* Kamati inaishauri Tume kuweka uwazi katika mfumo wa ajira ili wananchi wafahamu kila hatua inayopitiwa katika utoaji wa nafasi mpya baada ya kutangazwa.

## 3.9 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA)

Chuo cha Utawala wa Umma ni Chuo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilichopo chini ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Ubora. Chuo cha Utawala wa Umma kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 1 ya mwaka 2007.

Kiujumla, Chuo kimefanikiwa kutekeleza majukumu yake ya kuwaendeleza Watumishi wa Umma na Watumishi wa sekta binafsi kwa kuandaa Programu za mafunzo ya muda mrefu na mafunzo ya muda mfupi kwa vipindi tofauti.

Pia, Chuo kinatekeleza jukumu la kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika masuala mbalimbali yanayohusiana na Usimamizi wa Utawala wa Umma pamoja na kutafsiri mageuzi yanayotokea katika Utumishi wa Umma ili kuleta mabadiliko katika kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Aidha, Chuo kimefanikiwa kuhuisha hati ya Mashirikiano baina ya Chuo Kikuu cha Utawala wa Umma na Chuo cha Utumishi Tanzania (TPSC) ambapo pamoja na mambo mengine taasisi hizi zinashirikiana katika programu za mafunzo ya muda mrefu.

### Changamoto za Chuo cha Utumishi wa Umma (IPA)

Licha ya mafanikio ambayo Chuo kimeyafikia kwa mwaka huu, lakini bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)* Wanafunzi kutolipa ada ya masomo kwa wakati;

*(ii)* Kuchelewa kwa watumishi wapya kwenda kupatiwa mafunzo elekezi (induction course) kwa wakati;
*(iii)* Ubovu wa miundombinu kwa upande wa Chuo kwa Pemba;
*(iv)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Chuo cha Utumishi wa Umma (IPA)**

*(a)* Kamati ilipata kutembelea na kukagua eneo la Mfikiwa lenye kiwanja cha Chuo kwa upande wa Pemba na kuona changamoto zilizomo katika eneo hili. Kamati haikuridhishwa na eneo hili kwa ujenzi wa Chuo na hivyo, inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuzuia ujenzi ambao umepangwa kufanywa katika eneo hili na hivyo kutafuta eneo jengine ambalo litakuwa rafiki katika mazingira ya Chuo lakini pia halitaigharimu Serikali fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi.

*(b)* Ili Chuo kuweza kukusanya mapato na kujiendesha kama taasisi ya elimu, Kamati inashauri wanafunzi ambao hawalipi ada ya masomo kuzuiliwa matokeo yao ya mitihani au kuzuiliwa vyeti vyao vya masomo mpaka watakapokamilisha malipo ya ada.

*(c)* Kamati inshauri Chuo kutoa elimu na matangazo zaidi kwa taasisi za Umma juu ya umuhimu wa kupatiwa mafunzo elekezi pamoja na mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi.

*(d)* Chuo kizidishe kasi ya kutafuta wafadhili kwa ajili ya kujenga jengo la utawala ili kukidhi mahitaji ya Chuo katika ngazi za utawala.

*(e)* Kamati haikuridhishwa na maendeleo ya Chuo kwa upande wa Pemba na hivyo, tunashauri Serikali iwekeze zaidi katika kusimamia na kuimarisha maendeleo ya Chuo hiki kwa Pemba.

## 3.10 KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Kamisheni ya Utumishi wa Umma ni chombo cha kikatiba kilichoanzishwa chini ya kifungu cha 116 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 (Toleo la Mwaka 2010) na kifungu cha 17 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Nambari 2 ya Mwaka 2011, kama ilivyorekebishwa na Sheria Nambari 5 ya Mwaka 2012. Uanzishwaji wa Kamisheni hii ni moja ya jitihada za Serikali katika kuleta mageuzi katika Utumishi wa Umma kwa kusimamia Tume zote za Utumishi pamoja na kuratibu mambo mbali mbali ya Utumishi wa Umma ili kuwa na Utumishi wenye tija kwa wananchi.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeridhishwa na utendaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa namna ilivyofanikiwa katika kipindi hiki cha utekelezaji wa bajeti, mipango na miongozo kutoka Serikalini. Sambamba na hayo, Kamisheni imefanikiwa kuridhia na kupitisha miundo ya Taasisi mbali mbali za Umma ikiwemo Muundo wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utangazaji Zanzibar, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

### Changamoto za Kamisheni ya Utumishi wa Umma

Pamoja na mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika utekelezaji wa shughuli za Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:

*(a)* Kamisheni inakabiliana na changamoto ya kuimarisha Utumishi wa Umma ili kuwa na tija kwa kutoa huduma bora na mabadiliko ya fikra na utamaduni wa watumishi.

*(b)* Ukosefu wa fedha za matumizi mengineyo na hivyo kupelekea Kamisheni kushindwa kutekeleza mipango yake kwa wakati.

### Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma

*(a)* Maslahi ya watendaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma yaboreshwe ili kwenda sambamba na majukumu wanayoyatekeleza.

*(b)* Katika kujenga Utumishi ulio bora na wenye tija kwa wananchi, watendaji wa Serikali na Mashirika yasio ya Kiserikali ni lazima yakubaliane na miundo ya kiutumishi iliyopo ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

*(c)* Kamati inaishauri Kamisheni kuzifuatilia kwa kina Tume za Utumishi ili kuhakikisha zinatenda haki na zinawasimamia watumishi katika kutimiza wajibu wao kwa jamii.

*(d)* Kamisheni ihakikishe inaidhinisha miundo ya taasisi ambazo zina sababu za msingi kufanya mabadiliko na sio kufanya mabadiliko kwa kufuata utashi wa wakuu wa taasisi au kuangalia upande mmoja wa maslahi ya taasisi husika.

*(e)* Aidha, Kamati inaigiaza Kamisheni kufuatilia kikamilifu Taasisi zote ambazo zimeshaidhinishiwa miundo mipya na kuona utekelezaji wake. Hata hivyo, ni vyema ukawepo mpango maalumu wa ukaguzi kwa kila mwaka kwa taasisi

zote za umma.

## 3.11 AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG)

Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu namba 112 pamoja na Sheria Namba 11 ya mwaka 2003 ya Uanzishwaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo majukumu ya Afisi yameainishwa kwa kina kupitia Sheria hii.

Kamati imeridhishwa na utendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kutokana na mafanikio makubwa ambayo yamepatikana. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuimarisha mashirikiano na taasisi nyengine za Umma na kuweza kutekeleza ukaguzi wa pamoja katika taasisi mbalimbali ikiwemo ukaguzi wa Miradi ya fedha za UVIKO, ukaguzi wa Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato (TRA), ukaguzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ukaguzi wa vyama vya siasa, ukaguzi wa miradi ya TASAF pamoja na Ukaguzi wa Balozi mbalimbali za Tanzania.

### Changamoto za Afisi ya CAG Zanzibar

Katika taarifa ambayo Kamati imeipokea kutoka Afisi ya CAG imeweza kubaini changamoto mbali mbali ambazo zimekuwa zikifanywa katika taasisi za Umma na binafsi. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatavyo:

*(i)* kuwepo kwa upotevu wa Majalada au baadhi ya taarifa muhimu kwa baadhi ya wastaafu waliotumikia utumishi wao zaidi ya taasisi moja katika Serikali na kukosekana kwa baadhi ya vielelezo muhimu katika majalada ya wastaafu mfano; mikataba, aridhilhali, barua za vizuizi vya mishahara vithibitisho vya kifo, barua za bodi ya madaktari nk;

*(ii)* ujazwaji usioridhisha wa taarifa za mishahara katika kalamazuu na kupelekea kukosekana kwa usahihi wa taarifa za hesabu za mafao kwa baadhi ya wastaafu;

*(iii)* Kukaguliwa kwa gharama kubwa zaidi ukilinganisha na uwezo wa ofisi na uhalisia wa kazi ulivyo;

*(iv)* upatikanaji wa fedha za (OC) hauwendani na utekelezaji wa majukumu ya Afisi;

(v) ukosefu wa wataalamu wa ukaguzi katika kaguzi za kiufundi katika kuangalia ubora wa miundombinu ya skuli, hospital, dawa (wahandisi wa majengo, wafamasia na wakandarasi vipimo;

(vi) ukosefu wa vitendea kazi katika kazi za ukaguzi wa kiufundi (kupima ubora wa majengo).

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Afisi ya CAG Zanzibar**

(a) Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuboresha maslahi ya Ofisi ya CAG na hivyo kwenda sambamba na wakaguzi wengine wenzao wa Tanzania Bara.

(b) Kwa kuwa taasisi hii inajukumu la msingi katika kukagua na kudhibiti hesabu za Serikali, Kamati imeona ipo haja sasa kwa Serikali kumuwezesha CAG kufanya ukaguzi wa miundombinu, ukaguzi wa majengo ya Umma na ukaguzi wa vifaa vya kazi.

(c) Kamati pia, inaishauri Serikali kuangalia kwa kina umuhimu wa fedha za matumizi mengineyo kwa taasisi hii, kwani kiwango wanachopata hakilingani na majukumu yao.

(d) Kamati vile vile, inaishauri Serikali kuweka mkakati maalumu wa kuipatia taasisi hii usafiri wa uhakika ili iwe ni nyenzo muhimu katika kazi zao. Aidha, katika suala hili ni vyema CAG akapewa uwezo wa kununua gari zake mwenyewe badala ya kusubiri mgao kutoka Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango.

(e) Kamati pia, inaishauri Serikali kuiwezesha Ofisi kujiendesha kitaalamu kwa kupatiwa nyenzo na wataalamu watakao isaidia Serikali kuokoa fedha nyingi kupitia miradi ya maendeleo.

## 3.12 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO

Wakala wa Serikali Mtandao ni Taasisi iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao, Nambari 12 ya mwaka 2019. Lengo kuu ni kusimamia na kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Utumishi wa Umma na kuleta maendeleo ya haraka ya kiuchumi na kijamii. Katika kutekeleza majukumu yake ya msingi Wakala imeweza kuandaa miongozo ya usimamizi wa masuala ya TEHAMA katika sekta za umma kwa kutayarisha rasimu kumi na kuziwasilisha kwa wadau na kupata maoni yatakayosaidia kuimarisha miongozo hiyo.

Aidha, Wakala imefanikiwa kupitia nyaraka mbali mbali za kitaalamu pamoja na kutoa ushauri kwa taasisi zinazohitaji kufanya ununuzi au kuanzisha mifumo ya ununuzi kwa njia ya mtandao. Sambamba na hayo wakala imefanya mafunzo ya utumiaji wa mifumo mbali mbali ya kielektroniki kwa ajili ya kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi na utoaji wa huduma kwa jamii. Miongoni mwa mifumo hiyo ni ZanMalipo, eOffice, ZanAjira na Mfumo wa Bajeti na Matumizi ya Taasisi za Serikali (BAMAS).

**Changamoto za Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar**

Pamoja na kupatikana kwa mafanikio kwa Wakala wa Serikali kwa mwaka huu, lakini bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la wataalamu ambao wataiwezesha Taasisi hii kufanya kazi zake kiushindani na kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, hali hii imepelekea Wakala kuonekana ipo nyuma siku hadi siku kutokana na mifumo yake inayoianzisha kushindwa kufanya kazi kiufanisi zaidi.

*(ii)* Kwa upande wa uanzishaji wa mifumo; Wakala imeazisha na kusimamia mifumo mbali mbali ambayo msingi wake ni kuondosha mifumo ya zamani ambayo ilisababisha Serikali kupoteza mapato yake na kupata hasara. Kwa mfano mfumo wa ZanAjira umeazishwa kwa malengo mazuri lakini bado malengo hayajafikiwa na umesababisha vijana kadhaa kukosa haki yao ya kufanya maombi ya ajira kupitia mfumo huu.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

*(i)* Ili kufikiwa lengo na dhamira ya kuanzishwa kwa Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali kusimamia kikamilifu maendeleo ya Wakala na kuhakikisha Wakala umekuwa ukienda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia;

*(ii)* Kamati imebaini kuwa mifumo ya Serikali Mtandao inayotumika na Taasisi za Umma haina ubora na imekuwa ikileta ugumu wa kutoa huduma kwa wananchi. Hivyo, Kamati inashauri kabla ya kuanza kutumika kwa mifumo hiyo Wakala ianze kufanya majaribio na kukusanya maoni ya wananchi juu ya matumizi bora ya mifumo hiyo.

*(iii)* Kamati inashauri Wakala kutafuta na kupendekeza kuajiriwa wataalamu wenye uzoefu katika fani za IT ili kusaidia maendeleo ya teknolojia ya habari nchini.

*(iv)* Aidha, Wakala isimamie na ihakikishe Taasisi zote za Serikali zimefikiwa na mifumo stahiki ya mtandao ili kuweka uwiano wa kutoa huduma baina yao.

*(v)* Wakala isisite kuchukua hatua kwa Taasisi zote za Umma ambazo zitaenda kinyume miongozo ya matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika kutoa huduma kwa umma.

## 3.13 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar imeundwa kwa Sheria Namba 1 ya mwaka 2012 Sheria ambayo inakwenda sambamba na Sera ya Utawala Bora ya Mwaka 2011 ambayo msingi wake wa tatu ni Kuzuia Rushwa. Msingi huu umezingatiwa katika nyaraka tofauti zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2020, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini, na Mkakati Shirikishi wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi wa Zanzibar.

Katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka imeweza kufanikisha kwa kiasi kikubwa kukuza uelewa kwa wananchi wengi kusihirikiana na Mamlaka kutoa na kuripoti taarifa za vitendo vya rushwa vinavyotokea katika jamii, sambamba na hilo, Mamlaka imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuongeza mashirikiano na Taasisi za Serikali na Binafsi jambo ambalo linapelekea Mamlaka kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi.

### Changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu ya Uchumi Zanzibar

Licha ya mafanikio ambayo ZAECA imeyafikia, lakini bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)* amati imebaini kuwepo kwa changamoto ya vifaa vya kisasa vya kiuchunguzi katika kuimarisha mikakati ya kuzuia uhujumu uchumi katika maeneo kama ya bandarini na uwanja wa ndege Unguja na Pemba.

*(ii)* Vile vile, mamlaka inakabiliwa na changamoto ya jengo la ofisi kwa upande wa Kusini Pemba.

*(iii)* Kamati pia imebaini kuwepo kwa uhaba wa vyombo vya usafiri kama vile magari kwa ajili ya ufuatiliaji na uchunguji wa uhalifu.

*(iv)* Aidha, Mamlaka inakabiliwa na tatizo sugu la uhaba wa wataalamu katika fani tofauti jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo yake.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

*(i)* Kamati inashauri ZAECA kuzidi kuwaimarisha watendaji wake kwa kuwapatia elimu na mafunzo ya kutosha ya kukabiliana na uhalifu wa kuhujumu uchumi.

*(ii)* Kamati pia, inaishauri ofisi ya ZAECA kushirikiana kikamilifu na Taasisi ya Ubora wa Viwango Zanzibar – ZBS katika kudhibiti matumizi ya bidhaa zilizopitwa na wakati (expire date) hususan bidhaa za vyakula na vipodozi.

*(iii)* Kamati inaishauri Serikali kusaidia upatikanaji wa vyombo vya usafiri kwa ZAECA ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yao.

*(iv)* Kamati inashauri ZAECA kusimamia upatikanaji wa vitendea kazi vya kisasa kwa kusihirikiana na Serikali juu ya umuhimu wa vifaa hivyo katika kuimarisha maendeleo ya uchumi wetu.

*(v)* Aidha, Kamati inaishauri ZAECA kuhakikisha wamejipanga katika kudhibiti hatua za awali za kutenda rushwa na uhujumu wa uchumi katika Taasisi za Umma na Binafsi ili kuepuka kutumia nguvu kubwa kutokana na matendo hayo. Aidha, ni vyema kwa ZAECA kupatiwa asilimia ishirini na tano (25%) ya fedha wanazookoa kutokana na rushwa na uhujumu uchumi ili iwe ni njia moja wapo ya mapato kwa taasisi hii.

## 3.14 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni Taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria namba 4 ya Mwaka 2015 na imepewa mamlaka ya kusimamia maadili ya viongozi wa umma. Mamlaka hayo yanajumuisha kupokea, kusajili na kuhakiki Tamko la Rasilimali na Madeni kutoka kwa Viongozi wa Umma, kufanya uchunguzi na kushughulikia malalamiko, tuhuma au madai kuhusu uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kutoa elimu kwa umma na viongozi kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili.

**Changamoto zinazoikabili Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kamati wakati wa ufatiliaji wa utekelezaji wa kazi za imegundua bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa Wafanyakazi hasa wa fani na kada za Sheria na Uchunguzi.

*(ii)* Uchakavu wa jengo la Ofisi Pemba

**Maoni na Ushauri wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

(i) Kamati inashauri Wizara kuendelea na hatua za kuongeza watumishi wenye sifa zinazohitajika kutoka Taasisi za Serikali.
(ii) Kamati inashauri kuwatafutia Ofisi Tume ya Maadili kisiwani Pemba ambayo itaendana na hadhi ya Ofisi hiyo na kufanya kazi bila ya matatizo yoyote.
(iii) Kamati inashauri Tume ya Maadili kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake namna bora ya kuweza kudhibiti siri zinazotokana na ujazaji fomu.

## 4. OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kusimamia Sera, Sheria na Kanuni za Ofisi ili kuhakikisha kuwa inaweka mazingira mazuri ya kutoa huduma za kijamii na kiuchumi sambamba na kuimarisha ulinzi na usalama kwa wananchi na wageni wanaoingia na kutoka Zanzibar. Aidha, Ofisi hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zinazotekelezwa na Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO's) ambazo zinasaidia kupunguza umasikini na kukuza uchumi wa wananchi.

Dira ya Ofisi hii ni kuwa Taasisi imara katika kusimamia amani, usalama, usajili wa wakaazi na upatikanaji wa huduma karibu na wananchi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaundwa na Idara zifuatazo zilizo chini Katibu Mkuu:

*(a)* Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa.
*(b)* Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ.
*(c)* Tume ya Utumushi wa Idara Maalum za SMZ.
*(d)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(e)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
*(f)* Ofisi Kuu Pemba.

Aidha, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inasimamia Taasisi 11 zinazojitegemea zifuatazo: -

*(a)* Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU),
*(b)* Chuo cha Mafunzo (MF),
*(c)* Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM),
*(d)* Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU),
*(e)* Kikosi cha Valantia (KVZ),
*(f)* Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi,
*(g)* Ofisi ya Mkoa wa Kusini Unguja,
*(h)* Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja,

*(i)* Ofisi ya Mkoa wa Kusini Pemba,
*(j)* Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba,
*(k)* Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi hiki katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Kamati imefanikiwa kuzitembelea na kukagua utekelezaji wa kazi za taasisi mbali mbali zilizochini ya Ofisi hii.

Hivyo basi, kwa kutumia Kanuni ya za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020 – 2025), miongozo ya sera na matoleo mbali mbali ya Serikali pamoja na Ilani ya CCM ya 2020 – 2025, Kamati imeweza kutembelea na kukagua utekelezaji wa bajeti na miradi ya maendeleo kwa taasisi zifuatazo:

## 4.1 JESHI LA KUJENGA UCHUMI *(JKU)* ZANZIBAR

Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar *(JKU)* limeanzishwa chini ya kifungu cha *121(1)* cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* pamoja na Sheria nambari *6* ya mwaka *2003*. Kwa mujibu wa Sheria, JKU imepewa jukumu la kutoa mafunzo kwa vijana katika nyanja za uzalishaji wa kilimo, mifugo na uvuvi. Vile vile, Idara hii imepewa jukumu la kuwafunza vijana ufundi, kazi za amali na uzalendo kwa ajili ya kuwafanya vijana hao waweze kujitegemea, kuitumikia na kuijenga nchi.

Aidha, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao waliyopewa na kuwaendeleza vijana kuwa na uzalendo na wenye kuleta tija kwa jamii. Idara hii pia, imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto ya makaazi kwa askari wake na vijana waliopo makambini pamoja na kuboresha ustawi wao kwa ujumla.

Kamati inatoa pongezi kwa Wakala wa Ulinzi wa JKU kwa juhudi zake wanazochukua katika kuimarisha suala la ulinzi na usalama kwa viongozi wetu lakini pia kwa wananchi wenye kuhitaji ulinzi au huduma kutoka kwa wakala. Sambamba na hayo, Kamati imeridhishwa na ulipaji wa madeni kwa Wakala ambayo walikuwa wakidai kwa muda mrefu kutoka taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kufanya Wakala waweze kutatua baadhi ya changamoto zilizowakabili kwa muda mrefu kutoka na ukosefu wa fedha.

### Changamoto za Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Zanzibar

Katika utekelezaji wa kazi za JKU Zanzibar na kutimiza malengo yaliyoainishwa

katika bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022, Kamati imebaini kuwa zipo baadhi ya changamoto zinazokifanya kikosi hiki kufikia malengo yake kwa hatua isiyo ya kuridhisha. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo: -

*(i)* Uwepo wa miundombinu ya barabara isiyo rafiki kwa kambi mbali za Unguja na Pemba;

*(ii)* Mabadiliko ya tabianchi na jinsi yanavyoathiri shughuli za kilimo, kwa mfano bonde la kilimo Kwapweza Wilaya ya Chake – Chake kushindwa kuendelea na uzalishaji wa mpunga kutokana na ukosefu wa maji.

*(iii)* Uhaba wa wataalamu wa mifugo na kilimo. Kamati imebaini kuwa JKU jeshi la kujenga Uchumi bado halijafikia malengo yaliyokusudiwa katika uzalishaji mali kwa muda mrefu sasa.

*(iv)* Kutokulipwa kwa fedha za muda wa ziada (over time) kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake wapiganaji wanaofanya kazi katika muda wa ziada.

*(v)* Upungufu wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi kwa ujumla. Hali hii inahusisha pia ukosefu wa matrekta na pembejeo nyengine za kilimo katika kambi zetu zote za uzalishaji.

*(vi)* Wapiganaji wengi kutokupatiwa likizo zao za mwaka kwa wakati pamoja na kutolipwa fedha za likizo kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa JKU Zanzibar**

*(i)* Kamati inashauri JKU kusimamia kikamilifu kazi za uzalishaji mali kwa kambi za mashamba kwa lengo la kufikia malengo yaliyokusudiwa.

*(ii)* Kamati pia, inashauri JKU kujikita katika ufugaji wa aina moja tu kwa kila kambi kulingana na mazingira ya kambi husika na waachane na kufuga bila

kuzingatia aina ya mifugo na tija inayopatikana.

*(iii)* Kamati inashauri JKU kuanzisha miradi mikubwa ya umwagiliaji katika kukabiliana na changamoto za tabianchi. Aidha, ni vyema Serikali kuangalia upya mradi wa umwagiliaji wa bonde la Cheju na uwezekano wa mradi huu kupewa JKU ili kuimarisha zaidi.

*(iv)* Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhakikisha kuwa wapiganaji na watendaji wote wanaostahiki kisheria kulipwa fedha za muda wa ziada wanalipwa ili kutowanyima haki zao za msingi na kuwajengea ari ya utendaji wao.

*(v)* Kamati inashauri JKU kusimamia upatikanaji wa samani katika majengo mapya yaliyojengwa ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha mazingira ya askari wetu.

*(vi)* Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kushughulikia upatikanaji wa likizo za wapiganaji wa JKU pamoja na kulipwa fedha zao za likizo kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

*(vii)* Mwisho, Kamati inashauri Serikali baada ya kukamilisha zoezi la ujenzi wa nyumba za askari sasa iangalie kwa umuhimu wake upatikanaji wa usafiri wa uhakika kwa JKU Unguja na Pemba ili kuondosha changamoto hii ya muda mrefu.

*(viii)* Kamati inashauri JKU kutafuta eneo jipya kwa ajili ya kuanzisha skuli nyengine ya sekondari ili kuongeza kasi ya udahili wa wananfunzi wanaohitaji kujiunga chuoni hapo.

## ZIARA YA KAMATI KATIKA KAMBI YA JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT) CHITA – MOROGORO

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kushirikiana na uongozi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa pamoja Uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) walifanikiwa kufanya safari ya kutembelea Kambi ya JKT Chita kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa na Jeshi hilo kwa upande wa Tanzania Bara mkoa wa Morogoro.

Pamoja na mambo mengine, Kamati ilifanikiwa kujifunza mambo kadhaa ikiwemo uzalishaji wa mazao ya chakula na ufugaji wa samaki. Katika ziara hiyo, Kamati ilipata kuelewa mbinu na mikakati iliyopangwa katika kuinua uchumi wa jeshi pamoja na utayari wao wanaouonesha katika kukuza maendeleo ya Taifa.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa JKU kutokana na ziara hii**

*(a)* JKU tunawashauri kuwekeza zaidi katika miradi ya maendeleo ya kilimo na mifugo kama jukumu lao kuu hapa Zanzibar.
*(b)* JKU lianzishe kampeni maalumu ya kambi zake kushughulikia uzalishaji kwa kila kambi kuwa na kipaumbele cha aina moja ya kilimo au mifugo ambayo itaendana na mazingira ya kambi husika.
*(c)* JKU ishirikiane na Wizara ya Kilimo ili kufanya utafiti wa mazao gani au mifugo gani inastawi katika kambi husika na sio kulima au kufuga kwa kubahatisha.
*(d)* JKU iombe ajira za wataalamu wa Kilimo ambao watasaidia kubuni na kuibua miradi mipya ambayo itakuwa mkombozi wa maendeleo yao.
*(e)* Kamati pia, inaishauri Serikali kuandaa fungu maalumu la bajeti kwa ajili ya kusaidia kuanzisha miradi ya maendeleo kwa kikosi cha JKU ambacho bila ya fedha hakiwezi kutekeleza mradi wowote wa maendeleo.

## 4.2 WAKALA WA ULINZI WA JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Wakala wa Ulinzi JKU ni Taasisi ya uzalishaji mali inayotoa huduma ya Ulinzi kibiashara kwa Taasisi za Serikali na watu binafsi, Jumuiya na wawekezaji waliopo Zanzibar kwa lengo la kuwekeza. Wakala imeanzishwa kwa agizo la Mheshimiwa Rais wa awamu ya saba (7) Dr. Ali Moh’d Shein kwa Mujibu wa Sheria Namba 2 ya Mwaka 2015.

**Changamoto za Wakala wa Ulinzi wa JKU Zanzibar**
katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku Wakala inakabiliwa na changamoto ndogo ndogo ambazo Kamati imezibaini na zinafaa kuchukuliwa hatua. Changamoto zenyewe ni kama zifuatavyo:

*(a)* Ufinyu wa Nafasi za Ofisi ya kufanyia kazi za Wakala;
*(b)* Kuchelewa kuondoka walinzi Makao Makuu siku ambazo kuna vikao jambo ambao huleta usumbufu kwa wateja;
*(c)* Uchakavu wa magari yanayowapeleka walinzi vituoni;
*(d)* Kukosekana kwa gari la dharura lenye viashiria juu;
*(e)* Kukosekana kwa askari wa akiba wa wakala wa ulinzi;

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Wakala wa Ulinzi**

*(i)* Kamati inashauri kuingizwa katika Programu za miradi ya maendeleo ili kuweza kupatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi zake.

*(ii)* Kamati inashauri Wizara kutafuta utaratibu mzuri wa kuwapatia mafunzo askari wake kila inapohiotajika kwa lengo lakuondosha migogoro inayojitokeza baina ya walinzi na wapewa huduma.

*(iii)* Kamati inaishauri Wizara kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuboresha kazi zao.

## 4.3 CHUO CHA MAFUNZO (MF) ZANZIBAR

Chuo cha Mafunzo *(MF)* Zanzibar ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria nambari *1* ya mwaka *1980* na Sheria nambari *3* ya marekebisho ya mwaka *2007*. Idara hii ina jukumu kubwa la kuwapokea wale wote wanaoletwa Chuo cha Mafunzo kwa mujibu wa Sheria, kuwalinda pamoja na kuwarekebisha tabia ili wanaporudi katika jamii wawe raia wema.

Kamati inaungana na wakuu wa Chuo cha Mafunzo kwa kutumia juhudi zao za kuwalinda na kuwaelimisha wanafunzi na mahabusu wanaoingia vyuoni baada ya kupata hukumu kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Aidha, Kamati imeridhishwa na utendaji kazi wa Idara hii kutokana na mafanikio makubwa yanayopatikana katika Idara hii na hivyo, kuweza kufikia katika viwango vya Kimataifa na kuwa mfano bora wa kuigwa kwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki.

**Changamoto za Chuo cha Mafunzo Zanzibar**

Licha ya mafanikio mazuri yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Chuo cha Mafunzo Zanzibar kimekabiliwa na Changamoto zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo na fedha za kuendesha kazi za maendeleo, kwa mfano zoezi la ufugaji wa samaki katika Kituo cha Bumbwini limekufa kutokana na ukosefu wa fedha za uendeshaji.

*(ii)* Athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo imesababisha shughuli za kilimo kusimama na hivyo kupungua kwa chakula kwenye makambi, kwa mfano Chuo cha Mafunzo Langoni ikitegemea maji ya chemchem ili kumwagilia

mashamba ya mpunga na mboga mboga ambayo kwasasa imekauka na imepelekea ukame mkubwa wa maji katika eneo hilo.

*(iii)* Kuwepo kwa uchakavu wa gereza la Kiinua Miguu ambalo limejengwa tangu enzi za wakoloni linapelekea kuvuja na kuhitaji fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati.

*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa mrundikano mkubwa wa mahabusu katika Gereza la Kiinua Miguu na Gereza la Wete unaotokana na mwenendo mdogo wa kesi Mahakamani (proceeding).

*(v)* Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa uchakavu wa vitendea kazi, mfano magari mengi ni mabovu na hayakidhi mahitaji ya Chuo cha Mafunzo kwa sasa.

*(vi)* Upungufu wa vifaa tiba hasa vya uchunguzi wa afya za binaadamu ni tatizo kwa upande wa huduma za afya.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Chuo cha Mafunzo**

Katika kukabiliana na changamoto hizo Kamati inashauri yafuatayo:

*(i)* Wizara kuchukua juhudi za makusudi za kusaidia Idara hii iweze kupata fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kusaidia kuendeleza miradi iliyokwama kutokana na changamoto ya fedha.
*(ii)* Kamati inashauri kiwango cha mahabusu wanaopelekwa gereza la Kiinua Miguu kipunguzwe na badala yake Mahabusu wengine wapelekwe gereza la Hanyegwa Mchana ili kupunguza msongomano.
*(iii)* Kamati inashauri Serikali ione uwezekano wa kutumia adhabu mbadala ikiwemo vifungo vya nje ni utaratibu wa kisheria na kawaida hivyo, kuwepo usimamizi maalum wa kutoa adhabu mbadala na kuzisimamia ili kupunguza mrudikano wa wanafunzi vyuoni.
*(iv)* Kamati inashauri Serikali kuwapatia usafiri Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya kuwapelekea na kuwarudisha wanafunzi pamoja na mahabusu Mahakamani ili kulinda usalama wao.
*(v)* Kamati inashauri Chuo cha Mafunzo kuyafanyia kazi yale yote waliyojifunza Tanzania Bara na pia kufanya ziara za mafunzo ya mara kwa mara kwa wataalamu wake ili kupata ujuzi wenye tija.

**ZIARA YA KAMATI KATIKA GEREZA LA MTEGO WA SIMBA KPF – MOROGORO**

Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilifanikiwa kuandaa safari ya kwenda katika **Gereza la Mtego wa Simba KPF** katika Mkoa wa Morogoro na kujifunza mambo kadhaa ambayo yanatekelezwa na Jeshi la Magereza katika Mkoa wa Morogoro.

Miongoni mwa mambo mazuri na ya msingi ambayo Kamati ilijifunza ni pamoja na:

*(a)* Kujengwa mazingira wezeshi kwa askari katika kuwatumikia wafungwa na mahabusu;
*(b)* Kujikita katika mifugo ya ng'ombe wa maziwa kama sekta ya uzalishaji mali;
*(c)* Kuandaa malisho kwa ajili ya ng'ombe ili kukabiliana na vipindi vya ukame;
*(d)* Kujenga na kuendesha kiwanda cha kusindikia maziwa na mtindi ili kudhibiti uzalishaji wa maziwa;
*(e)* Kuwepo wataalamu maalumu wa mifugo ambao wamepatiwa mafunzo katika vyuo vya Kilimo.
*(f)* Kuwepo bajeti kubwa ya gereza yenye kulenga uimarishaji wa mifugo na miradi mengine ya uzalishaji kama vile kiwanda cha matofali ya saruji na matofali ya udongo.

Kwa kuwa katika ziara hii, Kamati iliambatana na viongozi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Kamishna wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar na maafisa wake na kwa kuwa lengo la Kamati ilikuwa kujifunza namna wenzetu wanavyoendesha shughuli zao katika magereza; Kamati hii inaishauri Serikali kuunga mkono juhudi za Chuo cha Mafunzo katika sekta za uzalishaji kwa kuwapatia msingi (fedha) wa kutosha wa kuanzisha na kuendesha miradi ya maendeleo kitaalamu jambo ambalo ndio chanzo cha maendeleo yote katika Chuo.

Kamati pia, inaishauri Serikali kuwapatia wataalamu au kusomesha wataalamu ambao watahusika moja kwa moja na miradi ya maendeleo kwa Chuo cha Mafunzo ili kusaidia kuimarisha mikakati ya uzalishaji.

## 4.4 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo *(KMKM)* kimeanzishwa chini ya Sheria nambari *1* ya mwaka *2003* ambapo kina majukumu ya kulinda usalama wa bahari ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, kuzuia njia zote zinazoweza kutumika kupitishia magendo, kusaidia vyombo vya baharini vya abiria na kufanya uokozi baharini pamoja na kushirikiana na Jeshi la Wananchi pale

itakapotakiwa kufanya hivyo katika kuilinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kikosi cha KMKM kimefanikiwa kuimarisha shughuli za Ulinzi wa Bahari na nchikavu kwa kufanya doria mbali mbali na kufanikiwa kukamata baadhi ya mali za magendo katika juhudi za kupambana na uhujumu wa uchumi.

Vile vile, KMKM wamefanikiwa kuimarisha makaazi bora kwa Maafisa na Wapiganaji wake katika hatua ambayo Kamati inapongeza sana juhudi za Serikali kwa kuimarisha makaazi ya Askari wake pamoja na ofisi kuu ya Kamandi ya Pemba.

Aidha, Kikosi kimefanikiwa kutoa huduma bora za afya kwa Askari na raia wa mijini na vijijini pamoja na kuimarisha huduma kwa Hospitali kuu ya KMKM Mtoni. Sambamba na hayo, Kamati imeridhishwa na madhari nzuri ya Makao Makuu ya kikosi Kibweni kwa namna walivyofanikiwa kujenga ukuta na kuimarisha mazingira ya nje ya Kambi.

### Changamoto za Kikosi cha KMKM Zanzibar

Licha ya mafanikio mbali mbali ambayo Kamati imeyaona pamoja na mikakati ambayo inatumika katika utekelezaji wa majukumu yao, KMKM hata hivyo imekabiliwa na changamoto zifutazo:

*(i)* Uhaba wa fedha za matumizi mengineyo (OC).
*(ii)* Uhaba wa fedha za kuanzisha miradi na uendeshaji wa miradi
*(iii)* Uhaba na ukosefu wa vyombo vya usafiri kwa kambi zote Unguja na Pemba.
*(iv)* Ubovu wa miundombinu ya barabara za kuingilia Kambini.

### Maoni na Ushauri wa Kamati kwa KMKM

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kufanya kila inavyoona inafaa kuwapatia fedha za matumizi mengineyo ili kujikwamua na changamoto za fedha.

*(ii)* Kamati inashauri kikosi kuzidisha bidii katika operesheni za baharaini ili kukabiliana na wafanya magendo.

*(iii)* Kamati inashauri kikosi baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi kuu Pemba kuelekeza juhudi zake ujenzi wa mahanga ya askari Kisiwani Unguja.

## 4.5 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi *(KZU)* kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria nambari 7 ya mwaka *1999* na kina jukumu la kusimamia shughuli zote za uzimaji moto na uokozi wa maisha na mali za watu, kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto kwenye Viwanja vya Ndege na Bandarini zinakwenda sambamba kulingana na masharti ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Kamati ilifanikiwa kutembela na kukagua maendeo mbali mbali yenye ya Kikosi hiki na kujionea baadhi ya shughuli zake ambazo zilipangwa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

**Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa shughuli za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Zanzibar**

*(a)* Kama ilivyo kwa lengo kuu la Kikosi hiki, Kamati imeelezwa kwamba kimefanikiwa kutoa huduma katika matukio yote ya ajali za moto na ajali nyengine na kuokoa maisha ya watu na mali zao kwa kushirikiana na raia wema waliokuwa karibu ya matukio.
*(b)* Kikosi kimeendelea kutoa elimu kwa taasisi za kiserikali na binafsi juu ya majanga ya moto na jinsi ya kujikinga.
*(c)* Kikosi kimeendelea kufanya ukaguzi katika taasisi mbalimbali za Serikali na Taasisi binafsi na kuona jinsi zilivyojipanga kukabiliana na hali za dharura za majanga ya moto.
*(d)* Katika kuboresha mazingira ya kazi, Kikosi kimeanzisha ujenzi wa jengo la ofisi katika eneo la Mahonda na kufikia katika hatua nzuri.
*(e)* Aidha, kikosi kimefanikiwa kujenga jengo moja la ofisi na maegesho ya gari la kuzimia moto katika kituo cha Wete Mnazimmoja.

**Changamoto za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar**

Pamoja na mafanikio ya kikosi hiki bado kuna changamoto kadhaa zinazowakabili ambazo zimekuwa ni endelevu kutokana na hali inavyokwenda siku hadi siku, miongoni mwa changamoto hizo ni hizi zifuatazo:

*(i)* Kamati katika ukaguzi wake uliofanya imebaini kuwepo kwa uchakavu mkubwa wa magari ya kuzimia moto hasa katika kituo cha Mwanakwerekwe, pia yapo baadhi ya magari hayafanyi kazi kutokana na kukosekana huduma za kitaalamu kwa magari hayo.
*(ii)* Kamati imebaini kuwepo kwa gari moja tu la kubebea majeruhi au wagonjwa katika uwanja wa ndege wa Pemba; gari ambayo ni chakavu, ya

muda mrefu na haiwezi kufanya kazi kutokana na uchakavu wake.

*(iii)* Kamati pia, imebaini kuwepo kwa tatizo la jamii kuchelewa kutoa taarifa kwa wakati linapotokea janga la moto katika makaazi ya watu.

*(iv)* Kamati imebaini kuwepo kwa uchache wa vituo vya kuzimia moto hali inayopelekea ugumu wa kufika eneo la tukio na kuchelewa kwa waokozi kutokana ujenzi holela usiofuata mipango miji.

**Maoni na Ushauri na Kamati**

*(a)* Kamati inashauri Serikali kuandaa mpango maalumu utakaowezesha KZU kupata magari ya kutosha ya kuzimia moto pamoja na vifaa vya kisasa vitakavyosaidia kupambana na majanga ya moto.

*(b)* Kamati inashauri kikosi kuzidisha kasi ya ujenzi katika Kituo cha Mahonda ili kukamilika kwa wakati ulikusudiwa.

*(c)* Kamaati imebaini kuwepo kwa ukosefu wa kituo cha Zimamoto katika wilaya ya Mkoani, hivyo, tunashauri kuazisha ujenzi wa kituo kama hiki katika Wilaya ya Mkoani.

*(d)* Kamati inakishauri kikosi kufanya ukarabati wa magari yake mara kwa mara ili kuwasaidia katika kazi zao za kila siku.

*(e)* Kamati inashauri kikosi kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa taasisi za umma na zile binafsi ili kupunguza upotevu wa maisha na mali za wananchi.

*(f)* Maafisa wa kikosi wapatiwe mafunzo ya kitaalamu mara kwa mara ili kupambana na majanga haya na kuepusha kutumia njia za kienyeji katika kufanya uokozi ili kunusuru maisha ya watu.

## 4.6 KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)

Serikali iliamua kuanzisha Kikosi cha Valantia Zanzibar *(KVZ)* kwa mujibu wa Sheria nambari *5* ya mwaka *2004* na kukipa majukumu ya kuweka amani na utulivu nchini, kupambana na janga lolote litakaloikumba jamii, kulinda viongozi na mali za Serikali pamoja na kufanya kazi za kijeshi kwa madhumuni ya kuzuia hali inayohatarisha ulinzi na usalama nchi yetu.

Katika utekelezaji wa shughuli zake, kikosi hiki kinapiga hatua kila uchao na hivyo kuleta ushindani mkubwa katika kuanzisha na kuendeleza miradi yake na vikosi vyengine ambavyo vimeanzishwa kwa miongo kadhaa iliyotangulia. Sambamba na miradi ya maendeleo, Kamati katika utafiti wake wa muda mrefu imeona kikosi hiki kinaenda kuwa cha kupigiwa mfano kutokana na mafanikio yake ambayo yamepatikana kwa muda mfupi na hivyo utekelezaji wake kuweza

kuridhisha chini ya Kamanda lutein Kanal Said Ali Shamhuna.

Kwa sasa, Kikosi kimefanikiwa kupata mradi ambao unahusika na ujenzi wa mahanga, nyumba za maafisa na ofisi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kamati imeridhishwa na maendeleo ya mradi huu na kuwataka viongozi wake kuzidi kusimamia miradi hii ili ikamilike kwa wakati. Ni imani ya Kamati kwamba kukamilika kwa mradi huu kutaondosha kabisa changamoto ya makaazi ya askari katika kambi zao pamoja na kuwepo ofisi mpya na za kisasa.

### Changamoto za Kikosi Cha Valantia Zanzibar

Kikosi cha Valantia Zanzibar tukijumuisha Unguja na Pemba kinakabiliwa na changamoto ndogo ndogo ambazo katika utekelezaji wa majukumu yake imekuwa zikirudisha nyuma mipango yao. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Kamati inashauri kikosi katika jitihada zake za kuibua miradi ya maendeleo wasiache pia kufikiria uimarishaji wa huduma za maji safi na salama katika kambi zake zote za unguja na Pemba.
*(ii)* Kuwepo kwa miundombinu isiyorafiki kwa barabara za kuingia makambini kwa mfano Kambi ya Mto wa Maji, Kambi ya Mwanyanya, Pangatupu na Muyuni kwa upande wa Unguja na Kambi ya Ndugu Kitu na Pujini kwa upande wa Pemba.
*(iii)* Ukosefu wa vituo vya afya katika makambi.
*(iv)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri kuanzia makao makuu na kambi zote za Unguja na Pemba.

### Maoni na Ushauri wa Kamati Kwa KVZ

*(i)* Kamati inashauri Serikali kuunga mkono jitihada za kikosi kwa kuwapatia fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa wakati na kwa mujibu wa matumzi yao ya kila mwezi ili wapate kutekeleza kazi zao kama walivyojipangia.
*(ii)* Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kutuma fedha za miradi ya maendeleo kwa kikosi ili kukamilisha kazi zao za ujenzi.
*(iii)* Kamati inashauri Kikosi kufanya juhudi za makusudi katika kupambana na changamoto ya ukosefu wa zahanati.
*(iv)* Kamati pia inashauri KVZ kuzidisha kasi ya kufanya marekebisho ya sheria yake ili kwenda na wakati.

## 4.7 KAMPUNI YA UJENZI YA SERIKALI

Kampuni ya Ujenzi ya Serikali "Zanzibar Construction Company Limited" (ZCCL) imeanzishwa chini ya Sheria ya Msajili Hazina namba. 6 ya 2021. Kwa mujibu wa Sheria, mmiliki (shareholder) wa Kampuni ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Kamishna wa Mitaji ya Umma aliopo katika Afisi ya Rais Fedha na Mipango. Aidha, usimamizi wa shughuli za kila siku za Kampuni upo chini ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (AR) TMSMIM.

Lengo kuu la kuanzishwa kwa Kampuni ya Ujenzi ya Serikali ni kuisaidia Serikali kuhakikisha kwamba Zanzibar inakua na majengo bora na ya kisasa ya Serikali na ya watu binafsi ambayo yamejengwa kwa viwango na kwa thamani halisi".

**Changamoto za Kampuni ya Ujenzi ya Serikali**

Wakati kamati ikiendelea kufuatilia taarifa za utekelezaji kwa mwaka huu, imeelezwa kwamba bado Kampuni inakabiliwa na changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa fedha mtaji wa kuendesha kazi za Kampuni;
*(ii)* Kampuni inakabiliwa na uhaba mkubwa wa wataalamu katika fani mbalimbali za ujenzi hasa za kiufundi;
*(iii)* Ukosefu wa jengo rasmi la kampuni kwa ajili ya kuendeleza kazi zao;
*(iv)* Upungufu wa vyombo vya usafiri ambavyo vitawawezesha kufuatilia majukumu yao;
*(v)* Ufinyu wa vifaa na mashine muhimu zinazotumika katika kazi za ujenzi;
*(vi)* Ukosefu wa mafunzo ya kukuza taaluma ya mafundi wanaotoka katika Idara maalumu za SMZ.
*(vii)* Uwepo wa taasisi za Serikali zinazodaiwa na Kampuni kwa muda mrefu.

**Maoni na Ushauri wa Kamati Kwa KVZ**

a) Kamati inaitaka Wizara kukaa na kampuni kwa ajili ya kufuatilia Taasisi zinazodaiwa ikiwemo JKU na ZURA;
b) Kamati inashauri kutafuta uwezekana wa kuwatafutia Kampuni eneo jengo kwa ajili ya kuendeleza kazi zao za Ofisi kwakuwa sehemu waliopo sasa sio rafiki kwa utendaji kazi;
c) Kamati inashauri Wizara kuiangalia kwa jicho la karibu Kampuni hii na kupewa kazi wanazostahiki badala kazi kupitia moja kwa moja katika vikosi.

## 4.8 OFISI YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mkoa wa Mjini Magharibi ni miongoni mwa Mikoa mitano ya Zanzibar ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 2(a) na Sheria Nambari 08/2018 Sheria ya Tawala za Mikoa. Kiutawala Mkoa wa Mjini Magharibi ni mkusanyiko wa Wilaya tatu; (Mjini, Magharibi 'A' na Magharibi 'B') na Shehia 121 ukiwa na jukumu la kusimamia na kutekeleza Sera, Sheria, Mipango na Miongozo ya Serikali.

Aidha, Kamati inaupongeza uongozi wa Mkoa huu kwa juhudi zake za kusimamia ulinzi na usalama ambapo ni chanzo kikuu cha kupata mafanikio ya utekezaji wa majukumu ya mkoa huu.
Kwa mnasaba huo, Kamati imeridhia utekelezaji wake kutokana na mafanikio yafuatayo:

*(a)* kuimarisha masuala yote ya Ulinzi na Usalama kwa wananchi na wageni wanaoishi ndani ya Mkoa huu.
*(b)* Mkoa umeratibu maagizo na ahadi mbalimbali za viongozi wa SMZ na SMT zilizotolewa wakati wa ziara zilizofanywa ndani ya Mkoa.
*(c)* kufuatilia na kusimamia miradi ya maendeleo ambayo ndio msingi wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.
*(d)* kufuatilia na kusimamia matukio ya udhalilishaji ambayo yamekuwa yakiripotiwa katika Ofisi ya Mkoa siku hadi siku.

## 4.9 BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR

Baraza la Jiji la Zanzibar lilianzishwa mwaka 2019 chini ya kifungu cha 18 cha Sheria Nambari 7 ya Mwaka 2014. Majukumu ya msingi ya Baraza la Jiji yameainishwa katika kifungu cha 19(a), (b), (c), (d), (e), (f), (g) na (h) cha Sheria hiyo. Katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza Kamati imeridhishwa na hatua iliyopo katika utekelezaji wake licha ya kugubikwa na changamoto kadhaa ambazo zinarudisha nyuma juhudi zao. Aidha, Kamati inaupongeza uongozi wa Baraza kwa kuboresha maendeleo ya jiji pamoja na kulifanya liweze kutambulika katika utekelezaji wa shughuli zake ndani na nje ya nchi.

### Changamoto zinazolikabili Baraza la Jiji la Zanzibar

Katika utekelezaji wa Bajeti, Baraza la Jiji la Zanzibar linaendelea kusimama na changamoto zake za muda mrefu ambazo kimsingi hazijapatiwa utatuzi, changamoto zifuatazo:

*(a)* Ukosefu wa jengo la kudumu la Baraza pamoja na vifaa vya kufanyia kazi na vyombo vya usafiri.

*(b)* Ukosefu wa vyanzo vya mapato katika maeneo ya Jiji.
*(c)* Uhaba wa wataalamu katika sekta ya Uchumi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

Kwa kuwa Kamati imebaini changamoto mbalimbali ambazo kimsingi zinarudisha nyuma maendeleo ya Jiji la Zanzibar tumeona ipo haja ya kupendekeza hatua ambazo zitaweza kusaidia kutatua changamoto hizo, miongoni mwa hatua hizo ni kama ifuatavyo:

*(i)* Serikali kuchukua hatua za makusudi kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Nam. 7 ya Mwaka 2014 ambayo itaweka muundo utakao liwezesha Baraza la Jiji kujitegemea katika eneo lake la kiutawala pamoja na kuwa na vyanzo vyake vya mapato bila kuwepo mgongano na taasisi nyengine.
*(ii)* Kamati inashauri Baraza kuendelea kubuni na kuibua vyanzo vya mapato na miradi ya kiuchumi na kijamii ambayo italiwezesha Baraza la Jiji kujikimu kwa kipato na hivyo kupata nguvu kiuchumi.
*(iii)* Baraza liandae mpango maalumu utakaowawezesha kupata ofisi yake ya kudumu pamoja na kuwa na wataalamu ambao watasaidia kukuza maendeleo ya Jiji.
*(iv)* Baraza lizidishe mashirikiano yake na Taasisi nyengine za Serikali na zile za binafsi kwa lengo la kukuza mahusiano ya kiutendaji na uzalishaji na kuboresha maendeleo ya Jiji.

## 4.10 BARAZA LA MANISPAA MJINI

Baraza la Manispaa Mjini limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria nambari 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na lina jukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji. Kamati hii imekuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kufuatilia utekezaji wa programu mbali mbali za utekelezaji wa majukumu ya taasisi hii na kuweza kujionea mafanikio tofauti yaliyosaidia kupiga hatua ya kimaendeleo.

Miongoni mwa mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:

*(i)* Kuimarisha usafi wa mji na haiba yake.

*(ii)* Kutoa elimu ya usafi katika jamii.
*(iii)* Kuimarisha mazingira bora ya wafanyabiashara wadogo wadogo.
*(iv)* Kuboresha vyanzo vya mapato na ukusanyaji wa mapato.

**Changamoto za Baraza la Manispaa Mjini**

Licha ya mafanikio mbali mbali yaliyofikiwa katika kipindi hiki, Baraza la Manispaa ya Mjini linakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa idadi ndogo ya wajasiriamali waliosajiliwa ukilinganisha na idadi kubwa ya wajasiriamali waliopo mjini.

*(ii)* Aidha, Kamati imebaini kuwa elimu hafifu inayotolewa kwa wajasiriamali na wafanyabiashara katika kulipa kodi ni miongoni mwa changamoto za ukusanyaji wa mapato ya Baraza la Manispaa Mjini.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

Kutokana na changamoto hizi ambazo Kamati imeziibua na kimsingi zinarudisha nyuma maendeleo ya Manispaa ya Mjini, Kamati inashauri na kupendekeza mambo yafuatayo:

*(i)* Baraza lizidishe kasi ya kuibua vyanzo vipya vya mapato katika maeneo yake ya mjini pamoja na kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kwa kuziba mianya yote inayopelekea kushuka kwa mapato.

*(ii)* Baraza lihakikishe limeendeleza zoezi la usajili wa wajasiriamali pamoja nakuwapatia vitambulisho vya kazi kwa mujibu wa maeneo yao ili kupunguza vijana wanaozurura mitaani.

*(iii)* Kamati inashauri Baraza lizidishe kasi ya usafi wa mji pamoja na ukusanyaji wa taka katika maeneo mbali mbali ya mji.
*(iv)* Kamati inashauri Baraza kuwatumia Madiwani wao katika utoaji wa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi na kuzidisha kazi ya usafi wa mitaani.

## 4.11 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “A”

Baraza la Manispaa Magharibi ‘A’ limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria nambari

7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji. Aidha, Kamati katika ziara zake mbali mbali imekuwa ikitembelea na kukagua miradi na kazi tofauti ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Manispaa hii na kujionea mafanikio ya utekelezaji wake ukiwa wenye kuridhisha kwa kiasi chake. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

*(a)* Kuimarisha usafi wa Mazingira;
*(b)* Kusimamia na kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wadogo wadogo;
*(c)* Kusimamia na kufuatilia ujenzi wa soko la Chuini ili kuongeza vyanzo vipya vya mapato.
*(d)* Kuanzisha ujenzi wa soko la Uwelezo.

### Changamoto zinazolikabili Baraza la Mji Magaharibi 'A'

Licha ya mafanikio ambayo Baraza limeyafikia kwa mwaka huu, lakini bado zipo changamoto ambazo zinahitaji mikakati maalumu ya kuweza kuzitatua. Miongoni mwao nikama zifuatazo:

*(a)* Uhaba wa taarifa za uhakika kwa walipakodi waliosajiliwa;
*(b)* Uhaba wa vitendea kazi ikiwemo magari ya taka na vifaa vya ofisini;
*(c)* Elimu ndogo kwa wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ya mji na maeneo ya kibiashara.
*(d)* Kuzuiliwa kwa mnada katika soko jipya la Uwelezo Makufuli.
*(e)* Kubuguziwa kwa wafanyabiashara wa madagaa katika eneo la Kihinani.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

*(i)* Baraza lihakikishe limeweka mfumo madhubuti wa usajili walipakodi na kuwapa elimu juu ya umuhimu wake katika kukuza uchumi wa nchi;
*(ii)* Baraza lianzishe mpango ambao utawasaidia kupata vitendea kazi kwa mashirikiano na Serikali kuu ili kufikia malengo iliyojiwekea.
*(iii)* Baraza lizidishe kasi ya usafi wa mazingira na kuielimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya vifungashio vya bidhaa na athari zinazotokana na matumizi holela ya mifuko ya plastiki;
*(iv)* Baraza liajiri wataalamu wa mapato na wahandisi wa ujenzi ili kusimamia miradi yao wanayoitekeleza.
*(v)* Baraza kwa kushirikiana na Serikali.

## 4.12 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"

Baraza la Manispaa Magharibi 'B' limeanzishwa kwa Mujibu wa Sheria nambari 7 ya Mwaka 2014, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na linajukumu la kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kutoa huduma za usafi wa mji na mazingira, kukusanya mapato, kusimamia na kutekeleza mpango mkuu wa mji. Katika utekelezaji wa majukumu ya Manispaa hii mafanikio kadhaa yamepatikana ambayo yanatokana na juhudi za utendaji wao kama timu lakini juhudi za watu binafsi. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kama yafuatayo:

*(a)* Kuimarisha usafi wa mji kwa kuendeleza programu za usafi siku hadi siku kupitia maeneo ya biashara na makaazi ya watu;
*(b)* Kuhamasisha ukusanyaji wa mapato kupitia vyombo vya habari na kutoa elimu kwa walipakodi;
*(c)* Kuendelea na zoezi la kuwasajili wajasiriamali na kuwapatia vitambulisho;
*(d)* Baraza limeendelea na zoezi la ukaguzi wa maeneo yaliyoombewa vibali kwa ajili ya ujenzi katika sehemu mbali mbali za Wilaya ya Mjini Magaharibi B.

### Changamoto za Baraza La Manispaa Magharibi 'B'

Yapo mafanikio kadhaa yaliyofikiwa na Baraza la Manispaa Magharibi 'B' kutokana na utendaji kazi wao ambao hauna shaka umefanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu za Manispaa, pia zipo changamoto ambazo zikipatiwa ufumbuzi maendeleo zaidi yataweza kufikiwa katika Baraza la Manispaa hii.

Miongoni mwa changamoto hizi ni kama zifuatavyo:

*(i)* Kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kama vile magari ya kuzolea taka na mashine za kisasa za ukusanyaji wa mapato.
*(ii)* Uelewa mdogo wa wananchi katika ukusanyaji wa kodi pamoja kutofanya malipo kwa wakati.
*(iii)* Ukosefu wa mipango miji ambao unakwaza zoezi la usafi na kusababisha kuenea kwa taka katika maeneo mbali mbali ya Baraza hilo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

Kwa kuwa Kamati imeridhishwa na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji

wa majukumu ya Baraza kwa kipindi hiki, pia haikusita kushauri mambo mbali mbali ambayo kimsingi yanadhamira ya kuimarisha maendeleo ya Manispaa hii, kwa hivyo, miongoni mwa mambo ambayo Kamati inashauri ni kama ifuatavyo:

*(i)* Baraza lisimamie ipasavyo zoezi la ukusanyaji wa mapato kwa kuvitumia vyema vyanzo vyake vya mapato na kwa mujibu wa taratibu wa kisheria bila ya kuwaonea wafanyabishara na wajasiriamali wadogo wadogo.
*(ii)* Baraza liandae mpango mkakati ambao utasaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa vitendea kazi ikiwemo magari ya taka ili kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa taka katika mji.
*(iii)* Baraza lizidishe programu za elimu ya usafi na kulipa kodi kupitia vyombo vya habari na maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu. Aidha, itakuwa vyema kama likiandaa vipeperushi ambavyo vitabeba ujumbe wenye kuhimiza usafi wa mazingira na ulipaji wa kodi.

## 4.13 OFISI YA MKOA WA KUSINI UNGUJA

Mkoa wa Kusini Unguja umeundwa kwa mujibu wa Sheria nambari *8* ya Tawala za Mikoa ya mwaka *2014.* Mkoa unatekeleza majukumu yafuatayo:

*(a)* kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali.
*(b)* Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

Katika utekelezaji wa majukumu ya Mkoa wa Kusini Unguja yamebainishwa katika sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 kama ilivyo kwa Mikoa mengine ya Zanzibar. Aidha, Kamati inampongeza Mkuu wa Mkoa huu kwa kusimamia vyema majukumu ya Mkoa kutokana na kuimarika kwa ulinzi na usalama wa raia na mali zao, lakini pia hata wageni wanaoishi Mkoa huu bado wanaishi kwa amani na utulivu wa hali ya juu.

Katika utekelezaji wa majukumu ya Mkoa huu, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwa ni pamoja na:

*(a)* Kusimamia na kuendeleza hali ya ulinzi na usalama kwa kuimarisha amani na utulivu kwa wananchi;
*(b)* Kuendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya, ajali za barabarani na matukio ya moto;
*(c)* Mkoa umefanikiwa kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na

Utekelezaji wa maagizo ya viongozi kupitia ziara ya Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi na kutembelea maeneo ya miradi ambapo utekelezaji wake upo katika hali ya kuridhisha;

*(d)* Mkoa umefanikiwa kupambana na mripuko wa maradhi ya shuruwa kwa watoto na kuwezesha jamii kupata chanjo ya surua kwa asilimia mia moja.

**Changamoto za Mkoa wa Kusini Unguja**

Katika jitihada za kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umasikini katika jamii, hatuna budi kukabiliana na changamoto ambazo zinatukwaza katika maendeleo yetu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri;
*(ii)* Kuibuka kwa maradhi ya shurua kwa watoto wa chini ya umri wa miaka mitano;
*(iii)* Kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa wanawake na watoto;
*(iv)* Kuibuka kwa vikundi vya vijana wenye kuhatarisha maisha ya wananchi maarufu kama *panyarodi.*

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mkoa wa Kusini Unguja:**

Kamati kujenga mustakbali uliobora na wenye kuleta ufanisi wa mafanikio ya wananchi wetu, hatunabudi kuishauri Serikali ya Mkoa huu kukabiliana na changamoto hizi.

Aidha, Kamati inashauri kama ifuatavyo:

*(a)* Mkoa uandae programu maalumu zitakazowasaidia kutatua changamoto za vyombo vya usafiri ikiwemo kupanga katika bajeti yake inayokuja na kutafuta suluhisho la kudumu kutoka Serikalini.
*(b)* Mkoa usimamie kikamilifu upatikanaji wa chanjo ya shurua nyumba hadi nyumba kama kampeni ya wizara ya Afya inavyoelekeza.
*(c)* Mkoa uendeleze juhudi zake za kupambana na makundi hatarishi yanayojitokeza katika jamii ili kulinda na kuendeleza amani kwa wananchi wetu na wageni.
*(d)* Mkoa udhibiti matamasha yanayofanyika katika maeneo yake na kufahamu uhalali wa kila tamasha na malengo yake. Aidha, Kamati inashauri kuwepo kwa muda maalum kwa kumaliza sherehe za usiku.

## 4.14 BARAZA LA MJI KATI

Baraza la Mji Kati ni miongoni mwa Serikali za Mitaa ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya Mwaka 2014 na imekasimiwa majukumu yake kwa mujibu wa sheria hiyo. Kamati imefuatilia vya kutosha utekelezaji wa majukumu ya Baraza na kujionea jinsi wanavyojitahidi katika kufikia malengo waliyokusudia.

Mafanikio yaliyopatikana katika Utekelezaji wa Baraza la Mji Kati ni kama yafuatayo:

*(a)* Kuimarisha programu za usafi wa mazingira kwa maeneo yote ya makaazi ya watu na yale ya kibiashara;
*(b)* Kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa kuhifadhi taka hatarishi na matumizi salama ya vyoo.
*(c)* Kukamilisha mradi wa ujenzi wa Soko la Dunga Kiembeni;
*(d)* Kuimarisha mazingira ya wajasiriamali na makundi maalumu ili yaweze kujikwamua na umasikini.

**Changamoto zinazowakabili Baraza la Mji Kati:**

Katika mafanikio makubwa yaliyopatikana na kuisaidia jamii kufikia maendeleo endelevu, Baraza la Mji Kati linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Ukosefu wa gari la kubebea taka na kuzipeleka jaa kuu Kibele.
*(ii)* Uhaba wa vyombo vya usafiri katika utekelezaji wa majukumu yao;
*(iii)* Mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa kiasi kikubwa yamewaathiri wakulima na wajasiriamali;
*(iv)* Uelewa mdogo wa wafanyabiashara katika kulipa kodi na kutumia mashine za ukusanyaji wa mapato.
*(v)* Kasi ndogo ya usajili wa wajasiriamali na kutoa vitambulisho.
*(vi)* Kuwepo kwa mgogoro kati ya utawala na waheshimiwa Madiwani.

**Maoni na ushauri wa Kamati:**

Ili kuweza kufikia hatua ya mafanikio katika Baraza la Mji Kati na kufikia hatua iliyokusudiwa, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

*(a)* Kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kutoa elimu kwa wafanyabiashara pamoja na kubuni vyanzo vipya vitakavyosaidia ongezeko la mapato.
*(b)* Baraza liwafikie wajasiriamali wadogo wadogo na kutatua changamoto zao ambazo zinarudisha nyuma maendeleo yao, sambamba na kuwapatia vitambulisho kwa wakati. Aidha, Kamati inashauri Baraza kufikiria kupunguza gharama za usajili kwa

kuweka kiwango ambacho kila mmoja ataweza kugharamikia.

*(c)* Kamati inashauri suala la usafi wa mji kuongezewa bidii na kuhakikisha kila mmoja katika jamii amewajibika kwa eneo lake katika kuweka mazingira safi na salama.

*(d)* Baraza lisimamie kikamilifu vikundi vya vijana wanaojitolea katika kuinua uchumi na kukabiliana na changamoto za ajira.

*(e)* Afisi ya Baraza izidishe mashirikiano na waheshimiwa Madiwani katika kusimamia na kubuni miradi ya maendeleo.

*(f)* Afisi ya Baraza isimamie kikamilifu maslahi ya Waheshimiwa Madiwani kwa kuratibu vizuri shughuli za vikao vya Baraza na kuhakikisha stahiki zao zinapatikana kwa wakati.

*(g)* Aidha, Kamati haikuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa vyoo vya skuli ya Uchukuni na hivyo, inaliagiza Baraza kuhakikisha ujenzi huu unakamilishwa kwa wakati na kumsimamia mkandarasi kutimiza makubaliano ya mkataba.

## 4.15 HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja ni miongoni mwa taasisi za Serikali za Mitaa ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Namba 8 ya Mwaka 2014.

Katika utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri hii, Kamati imeelezwa mafanikio yafuatayo:

*(a)* Kuimarika kwa usafi wa mazingira ya miji na vijiji.

*(b)* Kuwawezesha wajasiriamali kiuchumi kwa kusimamia mradi wa ujenzi wa jengo la Wajasiriamali Kitogani.

*(c)* Kuimarisha na kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa kusimamia vyema vyanzo vya mapato na kuzidisha kasi ya ukusanyaji kwa wakati.

*(d)* Kamati pia, imeridhishwa na mradi wa ujenzi wa eneo maalumu la wajasiriamali na wafanya biashara wa Wilaya ya Kusini katika eneo la Kitogani.

### Changamoto za Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja

Mbali ya mafanikio hayo ambayo Halmashauri imefanikiwa kuyapata lakini bado Kamati imebaini changamoto mbali mbali ambazo kimsingi zinafanana na Halmashauri nyengine za Zanzibar. Changamoto zenyewe ni kama zifuatazo:

*(i)* Uhaba wa vitendea kazi vya kisasa katika ukusanyaji wa mapato.

*(ii)* Uelewa mdogo wa wananchi katika ukusanyaji wa mapato na kulinda vyanzo vya mapato.
*(iii)* Uhaba wa vyombo vya usafiri kwa watendaji wa Halmashauri.
*(iv)* Uhaba wa watendaji wa Halmashauri hususan wataalamu wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha katika fani za miradi na mapato.
*(v)* Uwepo wa tatizo la wizi wa mifugo, ukosefu wa malisho na elimu ndogo ya ufugaji wa kibiashara kwa wakulima.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja**

*(i)* Kamati inashauri Halmashauri kutoa elimu zaidi juu ya ukusanyaji wa mapato na uendelezaji wa vyanzo vya mapato.
*(ii)* Halmashauri isimamie wajasiriamali kuweza kupata vitambulisho na kuwasajili wale wote ambao wamekamilisha taratibu za kisheria.
*(iii)* Kamati inashauri Halmashauri kuzidisha kasi ya usajili wa wajasiriamali ili kupata takwimu zao halisi na kuwafikia katika shughuli mbali mbali.
*(iv)* Kamati inaishauri Halmashauri kuzidisha usafi katika maeneo ya kitalii na kusimamia shughuli zote zinazofanyika katika maeneo yao.
*(v)* Kamati inashauri Halmashauri waandae programu maalumu ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo katika kuendeleza na kukuza biashara zao.
*(vi)* Aidha, Kamati inashauri uongozi wa Wilaya kwa kushirikiana Halmashauri kusimamia na kufuatilia kikamilifu kadhia ya wizi wa mifugo na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika. Vile vile Halmashauri ifanye bidii katika kutafuta wataalamu wa mifugo na sehemu za malisho kwa wafugaji wa vikundi mbali mbali vya ufugaji.
*(vii)* Kamati inaigiza Halmashauri kuzidisha kasi ya kufanya usafi katika maeneo yake ya kitalii na kuboresha maeneo yote ambayo yanatumika kwa biashara. Aidha, Halmashauri inaweza kutafuta vikundi vya vijana na kuwatumia kwa ajili ya kufanya usafi wa maeneo yake.

## 4.16 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mkoa wa Kaskazini Unguja ni miongoni mwa Mikoa mitano ya Zanzibar ambao umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* na una majukumu ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

Mkoa wa Kaskazini Unguja unajumla ya Wilaya mbili; Wilaya ya Kaskazini “A” na

Wilaya ya Kaskazini “B” pamoja na Halmashauri za Mabaraza ya miji; Baraza la Mji Kaskazini “A” na Baraza la Mji Kaskazini “B”.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar ilifanikiwa kutembelea Baraza la Mji Kaskazini “A” na Baraza la Mji Kaskazini “B” Unguja.

## 4.17 BARAZA LA MJI KASKAZINI “A”

Baraza la Mji Kaskazini “A” Unguja ni moja ya Mabaraza mawili yaliyomo katika Mkoa wa Kaskazini Unguja yalioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria namba 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa, uwezo wake, kazi na wajibu, muundo, mpangilio, fedha na mambo mengine yanayohusiana na utaratibu uliowekwa katika sheria hiyo. Baraza la Mji Kaskazini “A” limepata mafanikio mbali mbali kutokana na utekelezaji wake na usimamizi madhubuti ya fedha za bajeti.

Miongoni mwa mafanikio yake ni kama ifuatavyo:

*(a)* Kusimamia usafi wa mazingira ya miji na fukwe;
*(b)* Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
*(c)* Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vyanzo mbali mbali vya Baraza hili;
*(d)* Kuendelea kusajili na kuwatambua wajasiri amali; na
*(e)* Kuwasaidia wajasiriamali kwa kuwajengea mazingira rafiki ya kibishara.

### Changamoto Za Baraza La Mji Kaskazini “A” Unguja

Baraza la Mji Kaskazini ‘A’ Unguja, linakabiliwa na changamoto tofauti ambazo zinarudisha nyuma maendeleo yao, miongoni mwa changamoto hizo:

*(i)* Uhaba wa vyombo vya usafiri na vitendea kazi vya Baraza;
*(ii)* Uhaba wa watumishi katika fani mbali mbali ikiwemo wataalamu wabunifu katika masuala ya mapato na miundombinu;
*(iii)* Baadhi ya vyanzo vya mapato kuhamishiwa Serikali Kuu na Maliasili;
*(iv)* Mwamko mdogo wa wananchi juu ya ulipaji kodi kwa hiari.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

Kutokana na changamoto hizo ambazo Kamati wamezibainisha na kuzitolea ufafanuzi wakati wa ziara zake; Kamati bado inaendelea kushauri mambo yafuatayo:

*(a)* Baraza liwashirikishe wananchi kikamilifu katika mipango na ujenzi wa miradi ya maendeleo ili kufikia malengo ya miradi husika;
*(b)* Kamati inalishauri Baraza kufuatilia kikamilifu suala la upatikanaji wa vyombo vya usafiri kama taratibu zinavyoelekeza;
*(c)* Kamati inashauri miradi inayoibuliwa na Baraza ikamilishwe kwa wakati na ijengwe katika kiwango kinachofaa kwa kuwasimamia vyema wataalamu wa miradi hiyo. Vile vile, miradi ifanywe kwa kuzingatia mgawanyo wa Wadi zilizomo katika Baraza.
*(d)* Kamati inashauri Baraza kusimamia upatikanaji wa vitambulisho kwa wajasiriamali na kuzidisha kasi ya usajili ili kuwa na taarifa za uhakika.

## 4.18 BARAZA LA MJI KASKAZINI "B"

Baraza la Mji Kaskazini "B" Unguja ni moja ya Mabaraza mawili yaliyomo katika Mkoa wa Kaskazini Unguja yalioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria namba 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa.

Katika ziara za Kamati, tumebaini kuwepo kwa malalamiko ya Waheshimiwa Madiwani pamoja na uongozi wa Baraza na Serikali ya Wilaya kwa kutoridhika na ushirikiano wanaoupata kutoka Serikali ya Mkoa hasa katika ugawaji wa fedha za maendeleo na kujaza nafasi ya Mwenyekiti wa Baraza ambayo kwa muda mrefu ameshaondolewa madarakani.

Katika utekelezaji wa malengo ya Baraza kwa mwaka 2022/2023 Kamati yetu imeridhishwa na juhudi zilizochukuliwa na uongozi wa Baraza kwa ajili ya kuimarisha maendeleo yake. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni haya yafuatayo:

*(a)* Kuendelea kutoa huduma bora kwa jamii, ikiwemo kuwapatia taaluma wananchi juu ya usafi wa mazingira na ulipaji wa ada kwa hiari.
*(b)* Baraza kuendelea kusajili wajasiriamali wadogo wadogo kwa lengo la kuboresha maendeleo yao.

### Changamoto Za Baraza La Mji Kaskazini "B"

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, pia zipo changamoto zilizojitokeza katika

utekelezaji wa shughuli za Baraza, miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

*(a)* Kutopatiwa mgao stahiki na kuchelewa kupatiwa mgao wa mapato yatokanayo na rasilimali ya mchanga.
*(b)* Kuondoshwa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kupelekwa Serikali kuu.
*(c)* Kuwepo kwa uhaba wa vyombo vya usafiri katika kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika vyanzo vya mapato.
*(d)* Uwelewa na mwamko mdogo wa wananchi katika kutumia mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato na usajili wa wajasiriamali.
*(e)* Ukosefu wa mgao wa mapato kutokana na chanzo cha minara ya simu na leseni za biashara za vileo.
*(f)* Matumizi ya mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za mapato (kupitia mfumo wa ZanMalipo) unaathiri ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na utoaji wa taarifa (Report) kutokana na changamoto za mfumo.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

Katika kukabiliana na changamoto hizo juhudi na mikakati mbalimbali inahitajika ili kuona changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi katika hatua kwa hatua. Hivyo, basi Kamati inashauri mambo yafuatavyo:

*(a)* Kamati inashauri Wizara iondoe mgogoro uliopo baina ya uongozi wa Mkoa na Baraza lamMji kwa kuwashirikisha kikamilifu katika miradi ya maendeleo inayopelekwa katika Halmashauri zao. Aidha, Kamaati inaagiza Wizara ijaze nafasi ya Mwenyekiti wa Baraza la Mji Kaskazini 'B' ambayo ipo wazi kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita.

*(b)* Kamati imebaini kushuka kwa ukusanyaji wa mapato katika Baraza la Mji Kaskazini 'B' kutokana nan a kuchukuliwa kwa vyanzo vyaoi vya mapato kutoka Serikali kuu na Maliasili.
*(c)* Baraza la Mji Kaskazini 'B' liendelee na kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitasaidia kuongeza mapato na kuacha kutegemea chanzo kimoja cha mchanga.
*(d)* Baraza liendelee kutoa elimu juu ya ulipaji kodi kwa hiari.
*(e)* Baraza liandae na liweke kipaumbele kwa watumishi wake katika kupata elimu ili kukabiliana na changamoto ya wataalamu.
*(f)* Baraza lihakikishe imewashirikisha waheshimiwa Madiwani katika hatua zote za uandaaji wa miradi ya maendeleo na kuweka vipaumbele kwa pamoja.

## 4.19 OFISI YA MKOA WA KUSINI PEMBA

Mkoa wa Kusini Pemba umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* na una majukumu ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

Kamati imeupongeza Mkoa huu kwa kuona utekelezaji wa shughuli zake zikifanikiwa kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwafanya wakaazi wa Mkoa huu kuwa na Imani na upendo mkubwa wa nchi yao.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kutokana na juhudi za:

(a) Kuimarika kwa hali ya ulinzi na usalama katika mkoa.
(b) Utekelezaji wa mpango mkakati wa kitaifa juu ya kupambana na masuala ya udhalilishaji ya Mkoa.
(c) Utoaji wa huduma za utumishi na uendeshaji Mkoa.
(d) Kusimamia na kufuatilia miradi ya ahueni ya UVIKO 19 katika Wilaya ya Mkoani na Wilaya ya Chake – Chake
(e) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mradi wa ujenzi wa soko la samaki na matunda la Machomane.

### Changamoto Zinazoukabili Mkoa wa Kusini Pemba:

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku bado kuna changamoto ndogo ndogo ambazo Kamati imezibaini na zinafaa kuchukuliwa hatua. Changamoto zenyewe ni kama zifuatavyo:

(a) Uchakavu na ufinyu wa majengo ya Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya – Chake Chake na Mkoani.
(b) Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika Ofisi za Mikoa na Wilaya.
(c) Athari za mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima na wajasiriamali.
(d) Uwepo wa tabia mbaya za wizi wa mazao na mifugo kwa baadhi ya maeneo.
(e) Tatizo labaadhi ya wananchi kutolipa kodi kwa hiari pamoja na kutotoa risiti za mashine.

### Maoni na ushauri wa Kamati

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mpango wa kujenga ofisi za Wakuu wa Wilaya ili kupata makaazi bora pamoja na kuzikarabati nyumba wanazoishi au kujengwa mpya pale ambapo uwezo utakaporuhusu.
*(ii)* Kamati pia, inaiomba Serikali kuwapatia watendaji wa ofisi za Wilaya na Mkoa vifaa vya kazi ikiwemo vyombo vya usafiri ili kuimarisha mazingira yao ya kazi.
*(iii)* Kamati inashauri watendaji wa Mkoa kuzidisha kasi ya utendaji ili kumsaidia Mkuu wa Mkoa kwa kutoa huduma bora katika jamii.
*(iv)* Kamati pia, inashauri Mkoa kutoa elimu ya mara kwa mara kwa wananchi juu ya kulipa kodi kwa hiari na kujenga tabia ya kudai risiti na kutoa risiti.
*(v)* Kamati inauagiza Mkoa wa Kusini Pemba kuchukua hatua za makusudi kwa kuwafuatilia na kupambana na watu wenye tabia mbaya ya wizi wa mazao na mifugo ya wakulima.

## 4.20 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

Kama ilivyo kwa Halmashauri nyengine za Zanzibar; Baraza la Mji la Chake – Chake ni moja ya Mabaraza mawili yaliyomo katika Mkoa wa Kusini Pemba yalioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sheria namba 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa. Katika utekelezaji wa malengo ya Baraza kwa mwaka 2022/2023 Kamati yetu imeridhishwa na juhudi zilizochukuliwa na uongozi wa Baraza kwa ajili ya kuimarisha maendeleo yake.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni haya yafuatayo:

(a) Kuongezeka kwa kasi ya ukusanyaji wa mapato na kuongeza vyanzo vipya katika maeneo ya mjini;
(b) Kuimarika kwa huduma za uendeshaji na Kuwajengea uwezo wafanyakazi;
(c) Kuimarika kwa usafi wa mazingira katika maeneo ya Miji na vijijini;
(d) Kuyawezesha makundi maalum kujiimarisha kiuchumi;
(e) Kuendelea kwa ujenzi wa soko la samaki na matunda la Machomane; na
(f) Kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa soko la wajasiriamali Michakaini.

### Changamoto zinazolikabili Baraza La Mji Chake – Chake:

Pamoja na kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato pamoja kukuwa kwa hali ya

usafi wa Mji kwa kuzifikia Shehia nyingi zaidi bado Ofisi ya Baraza la Mji Chake – Chake inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadha wa kadha ambazo zinarudisha nyuma maendeleo ya Mji na Vitongoji vyake. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatavyo:-

*(i)* Mwamko mdogo wa wananchi katika ukusanyaji mapato kwa njia za kielektroniki.

*(ii)* Uhaba wa mashine za kukusanyia mapato na wataalamu wabobezi katika fani za mapato.

*(iii)* Ubovu wa gari la kukusanyia taka.

*(iv)* Kuchelewa kwa baadhi ya miradi ya maendeleo kutokana na mikataba dhaifu inayotengenezwa na Baraza.

*(v)* Ukosefu wa jaa la uhakika la kuhifadhia taka.

*(vi)* Ukosefu wa eneo la maegesho ya magari katika soko jipya la Michakaini.

### Maoni na Ushauri wa Kamati

*(a)* Kamati inalishauri Baraza kusimamia kikamilifu miradi yake ya maendeleo kwa lengo kulinda rasilimali za Serikali na wananchi.

*(b)* Kamati inashauri Baraza kufanya juhudi za makusudi kutafuta mtaalamu atayeboresha mfumo wa mashine za ukusanyaji wa mapato ili kuzuia mianya ya upoteaji wa mapato. Aidha, ni vyema kama Baraza litakuwa na mtaalamu ambaye atatumika kufanya marekebisho kila atakapohitajika.

*(c)* Kamati inashauri Baraza linapoingia mikataba ya miradi yake liwashirikishe kikamilifu wataalamu kutoka Ofisi Kuu Unguja pamoja na kupata baraka kutoka kwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*(d)* Baraza pia, lijikite katika usafi wa mji, ukusanyaji wa mapato na kutoa huduma kwa jamii kwani hizo ndio kazi kuu za Mabaraza kwa mujibu wa Sheria.

*(e)* Kamati inashauri Baraza kuwashirikisha kikamilifu waheshimiwa Madiwani

katika mipango ya Baraza pamoja na kuibua miradi ya kijamii.

*(f)* Kamati inashauri kujenga eneo la maegesho ya magari na bustani katika soko la Michakaini.

## 4.21 BARAZA LA MJI MKOANI – PEMBA

Katika muendelezo wa shughuli za Kamati katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali imefika Baraza la Mji Mkoani kama moja ya Mabaraza yaliyomo katika Mkoa wa Kusini Pemba lilioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji Sheria namba 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa. Katika utekelezaji wa malengo ya Baraza kwa mwaka 2022/2023 Kamati yetu imeridhishwa na juhudi zilizochukuliwa na uongozi wa Baraza kwa ajili ya kuimarisha maendeleo yake.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni haya yafuatayo:

*(i)* Kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya Mji;

*(ii)* Kulipa stahiki za wafanyakazi kwa wakati;

*(iii)* Kuimarisha bustani za mji ili kujenga haiba yake;

*(iv)* Kuyawezesha makundi maalum kujiimarisha kiuchumi.

### Changamoto zinazoikabili Baraza La Mji Mkoani

Licha ya Baraza kufanikiwa katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa ufanisi na uwazi zaidi lakini bado kuna changamoto mbali mbali zinazolikabili katika kufanikisha shughuli hizo kwa asilimia mia moja, miongoni mwa Changamoto hizo ni pamoja na:

*(i)* Upungufu wa fedha za matumizi mengineyo ukilinganisha na mahitaji yaliyopo;

*(ii)* Kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato katika vyanzo mbali mbali vya mapato;

*(iii)* Ufinyu wa Ofisi ukilinganisha na wafanyakazi waliopo ambapo hulazimika kila chumba kutumiwa na wafanyakazi zaidi ya wawili;

*(iv)* Uhaba wa vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri na gari la kuzolea taka pia ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

*(i)* Kamati inashauri Baraza kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ili kuimarisha miradi yake.

*(ii)* Kamati inalishauri Baraza kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza ufanisi wa makusanyo.

*(iii)* Ili kukabiliana na changamoto ya ufinyu wa nafasi, Kamati inashauri Baraza kutumia jengo la ofisi kwa kazi maalum na kazi nyengine zifanywe nje ya ofisi kama ni 'outreach programs'.

*(iv)* Kamati inalipongeza Baraza kwa kuimarisha usafi wa mji na kuwa katika hali nzuri lakini hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika kwa lengo la kuwa mfano bora kwa mabaraza mengine.

## 4.22 OFISI YA MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mkoa wa Kaskazini Pemba umeanzishwa chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari *8* ya mwaka *2014* na una majukumu ya kuratibu, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa sera, mipango na miongozo ya Serikali. Aidha, Mkoa unasimamia na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama na kuhakikisha kuwa rasilimali watu na vitu vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na jamii kwa ujumla.

Mkoa wa Kaskazini Pemba umeunganishwa na Wilaya Mbili (2), Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni pamoja na Wilaya ndogo ya Kojani.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Mkoa wa Kaskazini Pemba umefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

*(i)* Kuimarisha hali ya ulinzi na usalama wa Mkoa.

*(ii)* Kuimarika kwa kampeni ya mapambano dhidi ya udhalilishaji na ukatili ndani ya Mkoa.

*(iii)* Kuimarika kwa utoaji wa huduma za afya katika jamii.

*(iv)* Mkoa umejitahidi katika kusimamia mifumo ya elimu ili kwenda sambamba na sera ya taifa.

**Changamoto za Mkoa wa Kaskazini Pemba**

Aidha, katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Mkoa, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:

*(a)* Ufinyu wa nafasi za ofisi kulingana na idadi ya wafanyakazi.
*(b)* Ufinyu wa Bajeti kutokana na mahitaji ya ofisi.
*(c)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri.
*(d)* Kuwepo kwa kesi za wizi wa mifugo na mazao katika maeneo mbali mbali ya Mkoa.

**Maoni na ushauri wa Kamati**

*(i)* Kamati inashauri Mkoa kuzidisha kasi ya kuzisimamia Halmashauri zake kwa lengo la kuongeza kasi ya mapato na usafi wa miji.
*(ii)* Kuhusu suala la bajeti, Kamati inashauri Ofisi kufanya maombi kwa kufuata utaratibu maalumu wa maombi na kuyawasilisha katika wizara husika ili kupata nyongeza ya bajeti.
*(iii)* Kamati pia, inaishauri Serikali kuongeza fedha za matumizi maalum (Political Votes) kutokana na kiwango kidogo kilichopo ambacho kinaleta changamoto kwa waheshimiwa Wakuu wa Mikoa.
*(iv)* Mkoa uongeze kasi ya kusimamia na kufuatilia vitendo vya wizi wa mifugo na mazao ya wananchi.

## 4.23 BARAZA LA MJI WETE

Baraza la Mji Wete ni miongoni mwa taasisi za Serikali za mitaa ambazo utendaji wake umekuwa ukikua siku hadi siku kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha kwa kipindi kifupi cha miezi mitatu Baraza lilijipangia kutekeleza program kuu moja ikiwa ni Usimamizi na Uendeshaji wa Baraza la Mji Wete.

Katika utekelezaji wa Baraza la Mji Wete Kamati inalipongeza Baraza kwa hatua lzinazochukuliwa kukuza uchumi wake, miongoni mwa mafanikio yaliyofikiwa ni kama yafuatayo:

*(a)* Kuimarisha huduma za Mipango, fedha na rasilimali watu;
*(b)* Kuimarisha huduma za jamii na usafi wa mazingira;
*(c)* Kuyawezesha makundi maalum kuimarika kiuchumi na kijamii;
*(d)* Utekelezaji wa shughuli za Maendeleo kwa kusimamia miradi mbali mbali ikiwemo mradi wa ujenzi wa soko la wajasiriamali la Kifumbikai.

**Changamoto zinazowakabili Baraza La Mji Wete**

Afisi ya Baraza la Mji Wete inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(i)* Ukosefu wa gari la kukusanyia taka; na

*(ii)* Upungufu wa wataalamu husuan katika sekta ya mapato na majenzi.

**Maoni na ushauri wa Kamati**

*(i)* Kamati inalishauri Baraza la Mji Wete kuandaa mpango maalumu utakaowawezesha kupata vyombo vya usafiri ikiwa ni pamoja na kuwatumia wataalamu katika kuandaa miradi ya kimaendeleo kupitia nchi Wahisani na Taasisi za Fedha;

*(ii)* Kamati inashauri Baraza kufanya juhudi za makusudi katika kukuza mapato yake;

*(iii)* Baraza liongeze kasi ya kufanya usafi kwa maeneo yote ya wazi na yenye msongomano wa watu ikiwemo bandarini na hospitali ya Wete.

## 4.24 HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ni miongoni mwa Serikali za Mitaa iliyopo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba na imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sheria namba 7 mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa, Zanzibar. Halmashauri imekuwa mstari wa mbele katika kusimamia huduma za kijamii na kuhakikisha suala la mapato na usafi wa mazingira yake imekuwa kipaumbele siku hadi siku.

Katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanikiwa katika mambo yafuatayo:

*(a)* Halmashauri imefanikiwa kuibua na kusimamia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo;

*(b)* Halmashauri imeyawezesha makundi Maalumu kujiimarisha Kiuchumi na kijamii;

*(c)* Halmashauri imeweza kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo mbali mbali ya miji;

*(d)* Kuendeleza wigo wa udhibiti wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki.

*(e)* Kutoa elimu kwa jamii juu ya utunzaji, usafishaji na udhibiti wa mazingira na ulipaji wa kodi kwa hiari.

*(f)* Kutoa elimu kwa Wajasiriamali juu ya umuhimu wa kujisajili na kupatiwa vitambulisho.

**Changamoto zinazoikabili Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri.
*(ii)* Ukosefu wa magari ya kukusanyia taka.
*(iii)* Mwamko mdogo wa wananchi katika kulipa ada na tozo.
*(iv)* Wafanyabiashara waliowengi hawatumii mashine za risiti na hivyo kushindwa kutoa risiti kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

*(i)* Kamati inashauri Halmashauri kuendelea kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa wananchi ili kuzidisha kasi ya ukusanyaji wa mapato.
*(ii)* Kamati inashauri Halmashauri kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vyake ili kusaidia ongezeko la miradi ya maendeleo.
*(iii)* Kamati inashauri Halmashauri kuendelea kuwasajili wajasiriamali na kuwapatia vitambulisho kwa lengo la kufahamu mahitaji yao.
*(iv)* Halmashauri izidishe kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine za ukusanyaji na kutumia vyema vyanzo vya mapato.
*(v)* Kamati pia, inaridhishwa na ujenzi wa kituo cha Daladala cha Konde na inashauri ujenzi huu kukamilika kwa wakti ili kuongeza vyanzo vya mapato.

## 4.25 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar, nambari *3* ya mwaka *2018*.

Ofisi ya Wakala inatekeleza majukumu yake kama Ofisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbali mbali ya Serikali kwa lengo la kutoa huduma bora na endelevu kwa jamii.

**Mafanikio ya Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

*(a)* Kuimarika kwa huduma za usajili za ndani ya wakati (Timely Registration) hususan upande wa usajilio wa vizazi na vifo.

*(b)* Kuimarika kwa huduma za usajili wa Utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi (ZAN ID Online Registration) kwa wilaya zote za Unguja na Pemba.

*(c)* Wakala umefanikiwa kuingiza kumbukumbu za vizazi hai 60,000 katika mfumo wa usajili wa kielektroniki (Initialization Process) za kutoka mwaka 2014 hadi 2016. Hali ambayo imerahisisha upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa wakati ndani ya miezi mitatu ya Oktoba, Novemba na Disemba 2022.

*(d)* Kuongeza kifungu kipya cha mapato baada ya kuwapatia mafunzo ya elimu ya usajili wa ndoa na talaka kwa wafungishaji wa ndoa (Licenced Persons) ambao wanapatiwa kwa malipo maalum.

*(e)* Aidha, Kamati imeridhishwa na kiwango kilichofikiwa katika usajili wa matukio ya kijamii kupitia mfumo wa kielektroniki ambao unatumika katika kufanya usajili na hivyo kuweza kuhudumia wananchi waliowengi kwa muda mfupi.

**Changamoto zinazoikabili Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii katika utekelezaji wa majukumu yake inakuwa ikipambana na changamoto zifuatazo:

*(i)* Upungufu wa Wafanyakazi katika vituo mbali mbali hususan katika Wilaya ya Micheweni ambayo imeathirika zaidi katika utoaji wa huduma.

*(ii)* Ukosefu wa vyombo vya usafiri katika vituo vya Wilaya na ofisi kuu Unguja.

*(iii)* Ufinyu wa ofisi na ukosefu wa vitendea kazi kwa ofisi ya Wete ambapo hupelekea utoaji usioridhisha wa huduma kwa wananchi.

*(iv)* Wananchi wengi kutofika ofisi za vitambulisho na kuchukua vitambulisho

vyao vya Uzanzibari mkaazi.

*(v)* Mwamko mdogo wa wananchi kujisajili katika ndoa na talaka.

*(vi)* Wananchi wengi kutosajili matukio ya vifo mpaka wanapohitaji kwa ajili ya matumizi ya mirathi au mahitaji ya Serikali.

*(vii)* Bajeti ndogo ya Wakala na kuchelewa kupatiwa fedha za matumizi mengineyo kunaathiri mipango mikakati ya ofisi na kutofikia malengo kwa wakati.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Ofisi ya Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar**

*(i)* Kamati inaishauri jamii kuweka umuhimu katika usajili wa matukio ya kijamii ikiwemo vizazi, vifo, ndoa na talaka na vitambulisho.

*(ii)* Kamati inaishauri Serikali kuzidi kuziboresha ofisi za usajili wa matukio ya kijamii wilayani ili wananchi wapatiwe huduma za uhakika na kwa wakati.

*(iii)* Kamati inashauri Wakala kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa usajili ya matukio ya kijamii na faida zake kwa maendeleo ya nchi yetu.

*(iv)* Kamati inashauri Serikali kuwapatia Wakala fedha za matumizi kwa wakati na kwa kuzingatia maombi yao ili kutekeleza malengo ya kazi zao.

*(v)* Sambamba na hayo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza fungu la matumizi mengineyo kwa Wakala ili kutatua changamoto zao kwa kuwepo rasilimali fedha.

*(vi)* Mwisho, Kamati inawashauri watendaji wa Wakala kufanyakazi kwa uadilifu, busara na mashirikiano makubwa ili kutoa huduma zilizobora zaidi.

## 5. OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inashughulika na masuala mtambuka ya uhifadhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira, masuala ya watu wenye ulemavu, masuala ya VVU na UKIMWI na masuala yanayohusu udhibiti wa dawa za kulevya. Aidha, Ofisi hii inasimamia na kuratibu Ofisi ya faragha ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na masuala ya Sera, Mipango na Tafiti za Ofisi.

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaundwa na Idara zifuatazo:

*(a)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

*(b)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

(c) Idara ya Mazingira.
(d) Mamlaka ya Mazingira Zanzibar.
(e) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupamba na Dawa za Kulevya.
(f) Idara ya Watu Wenye Ulemavu.
(g) Ofisi ya Faragha.
(h) Ofisi Kuu Pemba.

## 5.1 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR (ZEMA)

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) imeanzishwa mwaka 2015 chini ya kifungu cha 14 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ya mwaka 2015. Lengo Kuu la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ni kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria, kanuni, miongozo na viwango vya mazingira kwa ajili ya kupunguza uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Aidha, Mamlaka ya ZEMA inasimamiwa na Bodi iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015. ZEMA imepangiwa majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015.

## 5.2 PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Programu hii inatekelezwa na Taasisi zote zinazosimamia masula ya kimazingira Zanzibar ikiwemo ZEMA ambapo utekelezaji upo kwa mujibu wa sheria ya Taasisi husika. Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa programu hii kwa vipindi tofauti ambapo nguvu zaidi inahitajika katika kufikia malengo yaliyopangwa.

Aidha, Kamati imeridhishwa na nguvu ya Mamlaka katika kuyarudisha maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi kwa kujenga ukuta na matuta ya kuzuia maji chumvi yasiingie katika maeneo ya kilimo pamoja na kufuatilia na kuyatambua maeneo yaliyolalamikiwa kutokana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Kamati ilipata fursa ya kuyatembelea maeneo yaliyoathirika zaidi ambayo ni Tovuni, Sipwese, Likoni, Kichanjaani Ndagoni pamoja na Mikindani Mtwara. Kamati imerishishwa na miradi hii na hivyo, tunaishauri Serikali kuhamishia nguvu zake za uhifadhi katika eneo la Kichanjaani Shehia ya Ndagoni.

Licha ya mafanikio mazuri yaliyopatikana kutokana na usimamizi wa uhifadhi mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa Mamlaka hii pia inajukumu la ukusanyaji wa mapato ambapo kwa kipindi cha Julai – Septemba 2022 ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tsh 78.8 milioni sawa na asilimia 112% za makusanyo.

### Changamoto ya Utekelezaji wa Programu

Changamoto kubwa ziliopo zinazohusiana na Sera, Sheria na mifumo ya kitaasisi katika Usimamizi wa mazingira, miongoni mwao ni kama zifuatavyo:

*(a)* Mwamko mdogo wa wananchi juu ya uhifadhi wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabianchi, hali hii inaonyesha kuongezeka kwa matumizi mabaya ya mifuko ya plastiki pamoja na kuharibu vyanzo vya maji kwa ukataji wa miti kiholela.
*(b)* Muingiliano wa baadhi ya sheria zilizopo juu ya usimamizi bora wa sheria ambao kwa baadhi ya maeneo hautoi wajibu wa moja kwa moja kwa taasisi husika hasa kwenye suala la uharibifu na uchafuzi wa mazingira ya baharini.
*(c)* Taasisi nyingi zinazohusiana na usimamizi wa mazingira na maliasili hazina uwezo mkubwa wa vifaa na teknolojia bora kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji wa mazingira.
*(d)* Wananchi kuendelea kuharibu mazingira bila kujali nguvu kubwa za Serikali ambazo zinatumika kuyarudisha mazingira katika uasili wake.

### Maoni na ushauri wa Kamati

Katika kuendeleza matumizi bora ya mazingira na uhifadhi wa mazingira katika jamii zetu suala utoaji wa elimu linahitajika zaidi ili jamii zifahamu umuhimu wake katika maisha ya kila siku. Pamoja na hilo, Kamati pia inashauri yafuatayo:

*(i)* Taasisi zenye jukumu la kusimamia uhifadhi wa mazingira zinapaswa kushirikiana bega kwa bega katika kuimarisha uhifadhi ya maeneo yetu.
*(ii)* Kamati inaendelea kushauri kufanyiwa mapitio ya Sheria zote zinazohusiana na mazingira kama vile Sheria ya misitu, Sheria ya usafiri baharini; na kutunga sheria mpya ya Madini itakayojumuisha pamoja na mambo mengine ya usimamizi wa maliasili zisizorejesheka.

*(iii)* Kwa kuzingatia umuhimu na uwezo wa wananchi wetu, tafiti zaidi zinahitajika juu ya nishati mbadala ya kuni na mkaa katika matumizi ya kupikia ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wa kipato cha chini.
*(iv)* Serikali izidishe kasi ya mapambano dhidi ya uingizaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki kwa Taasisi zinazohusika kuwachukulia hatua za kisheria wahusika. Aidha, Mamlaka iwashirikishe wananchi katika mapambano dhidi ya matumizi ya mifuko ya plastiki na vifungashio visivyo vya lazima katika bidhaa zetu.
*(v)* Vile vile, maeneo yaliyofaidika na kujengwa kuta za kuzuia maji bahari kuingia nchi kavu kama vile eneo la bandari ya Msuka, Likoni na Kengeja Sipwese

wananchi wanatakiwa kuyalinda maeneo hayo kwa kushirikiana na taasisi zenye mamlaka kama vile Manispaa na Halmashauri katika kuendeleza uhifadhi wa mazingira.

*(vi)* Aidha, Serikali inashauriwa izidishe fedha katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira kutokana na athari hasi za kila siku za mabadiliko ya tabianchi ili kwenda sambamba na malengo ya kitaifa na kimataifa katika kuhifadhi mazingira.

*(vii)* Kamati pia, inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kutekeleza vyama miradi ya uhifadhi wa mazingira katika maeneo ya Tovuni Wilaya ya Micheweni, Sipwese Wilaya ya Mkoani na Likoni katika Wilaya ya Wete. Vile vile, Kamati ilipata fursa ya kufika Mkoni Mtwara katika fukwe ya Mikindani na kuona namna miradi kama hii inavyotekelezwa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kamati inashauri miradi kama hii pia ifanywe katika fukwe ya Kichanjaani katika Shehia ya Ndagoni Pemba kutokana na athari kubwa za mazingira zinazoendelea kutokea.

## 5.3 PROGRAMU YA URATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Katika kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kuonesha Ulimwengu kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazopambana kikamilifu na biashara haramu ya dawa za kulevya; Serikali kwa mara nyengine iliamua kufanya maboresho ya sekta hii kwa kuanzisha Mamlaka inayosimamia Dawa za Kulevya. Aidha, Kamati imeridhishwa na sheria mpya ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 8 ya Mwaka 2021 ambayo imeanzishwa kwa lengo la kutoa uwezo kamili wa kudhibiti na kupambana na matumizi ya dawa za kulevya, usafirishaji, ugeuzaji wa kemikali bashirifu na udhibiti wa dawa tiba hapa Zanzibar.

### Changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar

Licha ya mafanikio mazuri yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar imekabiliwa na Changamoto zifuatazo:

*(i)* Kamati imebaini kuwepo kwa ukosefu wa vifaa vya kisasa vya utambuzi wa dawa za kulevya katika viwanja vya ndege na bandari zetu za Unguja na Pemba pamoja na uhaba wa GPS zitakazosaidia kugundua maeneo yenye wahalifu.

*(ii)* Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la uhaba wa ofisi za kisasa za Mamlaka

zenye majengo yanayoendana na hali halisi ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya, sambamba na uhaba wa rasilimali watu.

*(iii)* Jamii kujenga dhana potofu juu ya waathirika wa dawa za kulevya wanapotoka vituo vya kubadilisha tabia.

**Maoni na ushauri wa Kamati kwa Mamlaka**

Kutokana na changamoto hizo ambazo Mamlaka inakabiliana nazo katika mazingira mbali mbali, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

*(i)* Kamati inaishauri Serikali kuboresha maslahi ya watendaji wa Mamlaka ili kusaidia utendaji wao na kupunguza changamoto ndogo ndogo za kifedha.

*(ii)* Mashirikiano zaidi yajengwe baina ya jamii na Mamlaka ili kusaidia kupata taarifa za kudhibiti bandari bubu ambazo inasemekana kwa kiasi kikubwa zinatumika kupitishia dawa za kulevya kwa pwani ya Zanzibar.

*(iii)* Pia, ifikie pahala Mahakama iwe na idara maalumu ambayo itashughulikia kesi za Dawa za Kulevya pekee kama ilivyo kwa kesi za udhalilishaji ili kuziwezesha kesi kwenda kwa haraka.

*(iv)* Kwa kuwa Mamlaka hii ni mpya Serikali izidishe kasi ya kuioatia fedha kwa lengo la kutekeleza majukumu yake kwa urahisi na uhakika.

*(v)* Aidha, Kamati inaishauri jamii kujenga mazoea ya kuwaona waathirika wa Dawa za Kulevya kuwa ni watu wema na wenye kuaminiwa katika jamii baada ya kutoka vituo vya kurekebisha tabia.

## 5.4 TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Tume ya Ukimwi Zanzibar imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Ukimwi, nam. *3* ya mwaka *2002* ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kuhakikisha kuwa Mikakati ya Kitaifa, Sera na Miongozo itakayoongoza mapambano dhidi ya VVU na *UKIMWI* inaandaliwa pamoja na kupunguza makali ya virusi vya VVU na *UKIMWI* kwa kuhamasishana kuratibu utekelezaji wa Sera na Mikakati hiyo.

Kwa muda mrefu sasa Tume imekuwa ikiendeleza mapambano katika jamii na kuweza kuwafikia wananchi waliowengi kuwapa elimu juu ya madhara ya UKIMWI na jinsi yanavyoathiri uchumi wa Taifa. Kamati inaipongeza Tume kwa kuendeleza jukumu hili licha ya changamoto ndogo ndogo za kifedha ambazo zimetokana na mabadiliko ya uchumi wa Dunia.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

Kama ilivyo kwa maradhi mengine katika jamii jinsi Serikali kwa kushirikiana na washirika mbali mbali wanavyopambana kupunguza au kuyatokomeza kabisa, maradhi ya UKIMWI na VVU pia yanapaswa kuangaliwa kwa hatua madhubuti bila ya kuyachukulia kama maradhi ya kawaida katika jamii.

Hivyo, kutokana na Kamati kubaini kupungua kwa mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI katika jamii, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

*(i)* Elimu inahitajika kwa bidii kubwa katika jamii. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na NGO's ziendelee kutoa uelewa na kuihamasisha jamii kupitia mitandao ya kijamii, Redio, Televisheni na mikutano juu ya uwepo wa maradhi ya UKIMWI na athari zake kwa jamii na uchumi wetu wa ujumla.

*(ii)* Mapambano dhidi ya UKIMWI yasitumike kama fursa ya kujipatia kipato katika jamii bali yafanyike kama njia ya kupunguza maambukizi na athari za maradhi haya katika nchi yetu. Kufanya hivyo kutasaidia kufikiwa lengo lililokusudiwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

*(iii)* Serikali iiwezeshe Tume ya UKIMWI kushiriki kikamilifu katika mapambano kwa kuwapatia fursa mbali mbali ambazo zitaiwezesha Tume kuwa na nguvu na kufikia malengo endelevu.

*(iv)* Serikali iandae mkakati maalumu utakao komesha biashara haramu ya ngono katika nchi yetu. Aidha, jamii ifahamu kwamba mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ni jukumu la kila mmoja, hivyo ni wajibu wetu kuyaendeleza mapambano kwa kutojihusisha na vitendo vitakavyopelekea ongezeko la maambukizi mapya.

*(v)* Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti ya fedha kwa Tume ya UKIMWI ili kusaidia kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI.

## 5.5 BARAZA LA TAIFA LA WATU WENYE ULEMAVU

Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar limeundwa Chini ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Namba 8 ya Mwaka 2022 . Kamati imepata faraja kuona Baraza hili limepata Sheria mpya ya Watu wenye Ulemavu ambayo imeweka wazi haki na fursa za Watu hao katika jamii.
Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa kumteuwa Ndugu Ussi Khamis Debe kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu. Sambamba na hilo, Kamati inaipongeza Ofisi kwa kusimamia vyema programu ya Watu wenye Ulemavu na kuhakikisha wametekeleza majukumu yao kwa uweledi na ufanisi katika kuwahudumia watu wenye Ulemavu.

Baraza hili linafanya kazi kwa nia ya kuishauri Serikali juu ya maslahi yote na haki za Watu Wenye Ulemavu. Kamati imeridhisha na utekelezaji wa kazi za Baraza ambalo kwa kiasi kikubwa kwakuwa limefanikiwa kusikiliza malalamiko ya walengwa mbalimbali pamoja na kusimamia na kufuatilia masuala ya elimu mjumuisho katika jamii ili watu wenye ulemavu waweze kupata elimu kama watu wengine.

## 6. OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi imeanzishwa mwaka *2010* kutokana na mabadiliko ya *kumi na moja (11)* ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* toleo la *2010*. Jukumu la msingi la Wizara hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na masuala ya Muungano kwa upande wa Zanzibar.

Aidha, majukumu makhsusi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi ni pamoja na kutoa huduma bora kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais; kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa; kuandaa na kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa; kuratibu masuala ya Muungano; kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Tanzania Bara. Vilevile, inaratibu na kusimamia shughuli za Baraza la Wawakilishi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi inaundwa na Idara zifuatazo:

*(i)* Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais.

*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

*(iii)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

*(iv)* Idara ya Maafa.

*(v)* Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.

*(vi)* Idara ya Kuratibu Shughuli za Serikali.

*(vii)* Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ.

*(viii)* Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

Vile vile, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:

*(i)* Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW).

*(ii)* Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

## 6.1 BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni miongoni mwa mihimili *mitatu (3)* ya Serikali ambapo lilianzishwa kwa ajili yakustawisha demokrasia na uwakilishi wa watu wa Zanzibar. Majukumu makuu ya Baraza ni kutunga sheria, uwakilishi wa wananchi na usimamizi wa Serikali.

Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika kazi zake za msingi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar Mwaka 1984 ni kutunga sheria, kuihoji Serikali, kupitisha bajeti ya Serikali pamoja na kuidhinisha matumizi ya Serikali.

Ili kutekeleza vyema majukumu ya Baraza, Afisi ya Baraza la Wawakilishi imeandaa muundo mpya wa kiutumishi na kupitishwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa lengo la kuboresha utendaji na maslahi ya watumishi wake. Aidha, watendaji wamepangwa katika madaraja yao na kila mmoja amepata fursa ya kufahamu dajara lake kwa wakati. Kamati inaupongeza uongozi wa Afisi ya Baraza kwa hatua ya kupata muundo mpya. Aidha kupitia nafasi nauomba uongozi wa Afisi ya Baraza kuutumia na kuuendeleza vyema muundo huo mpya.

Vile vile, Kamati imeridhishwa sana na utekelezaji wa majukumu ya Baraza kwani limetekeleza ipasavyo malengo yake kwa kuratibu vikao vya Baraza pamoja na Kamati zake. Aidha masuali mbali mbali yaliratibiwa na kuulizwa kila Mkutano wa Baraza ambao ulifanyika kwa kipindi kilichopangwa.

Sambamba na hayo, Afisi ya Baraza imeendelea na kutoa mafunzo kwa watendaji wake kila baada ya muda ikiwa ni miongoni mwa mikakati inayofanywa kwa lengo la kuboresha utendeji kazi wa kila mtumishi.

### Changamoto za Baraza la Wawakilishi Zanzibar

Bila shaka kila lenye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto na hii ndio hatua muhimu ambayo itakufanya uweze kufikia mabadiliko. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

*(a)* Uhaba wa nafasi za ofisi kwa watendaji na wadau wakuu wa Baraza akiwemo Wakili Mkuu wa Serikali.
*(b)* Uhaba wa vyombo vya usafiri hususan gari za Kamati kwa Unguja na Pemba.
*(c)* Uchakavu wa majengo ya Ofisi kwa upande wa Pemba pamoja na ubovu wa Ukumbi wa Mikutano.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar**

*(a)* Kamati inashauri Serikali kuangalia kwa umuhimu wake suala la usafiri wa Kamati za Baraza ili kuendesha shughuli zake kwa ufanisi zaidi.
*(b)* Vile vile, Kamati inashauri suala la ujenzi wa jengo jipya la ofisi na kumbi za Kamati kuangaliwa kwa haraka ili kuweza kuboresha utendaji wa kazi za Baraza. Aidha, Kamati inashauri kuzingatio Afisi kwa ajili ya Mwanasheria mkuu kwa mustakbali wa kutekeleza vyema majukumu yake akiwa Barazani.
*(c)* Katika maboresho ya Afisi ya Pemba, Kamati inashauri Baraza kusimamia kikamilifu matengenezo ya Ukumbi mkubwa wa mikutano pamoja na ofisi zake ili kuweka mazingira bora ya utendaji na shughuli zote za Serikali zinazofanyika hapo. Aidha, Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Afisi ya Baraza Pemba kutokana na juhudi zao za kutoa huduma kwa waheshimiwa wajumbe pamoja kutekeleza vyema majukumu yao.
*(d)* Kamati inashauri Afisi ya Baraza izidishe kasi ya kutoa mafunzo kwa watendaji wake ili kupata watendaji wenye uzoefu na wanaoendana na wakati na mazingira ya mabunge.

## 6.2 TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Tume ya Uchaguzi Zanzibar ni chombo kilichoanzishwa mwaka *1979* chini ya kifungu cha *73* cha Katiba ya Zanzibar ya *1979*. Kwa hivi sasa Tume ya Uchaguzi Zanzibar inafanya kazi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya *1984*, Sheria ya Kuanzishwa kwa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, nam. 1 ya *2017*, Sheria ya Uchaguzi, nam. *4* ya *2018* na Sheria ya Kura ya Maoni, nam. *6* ya *2010*.

Miongoni mwa majukumu makuu ya Tume ni kukuza na kusimamia mienendo ya uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka huu wa 2022/2023 Tume ya Uchaguzi Zanzibar imefanikiwa vyema kutekeleza majukumu yake na hivyo kufikia ile azma kuu waliyoikusudia. Hata hivyo, Afisi hii imekabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha za matumizi jambo ambalo linarudisha nyuma utendaji wao.

**Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar**

*(a)* Kamati inashauri Tume kutafuta eneo bora lenye kulingana na umuhimu wa majukumu yake katika ujenzi wa ofisi za Wilaya hususan katika Wilaya ya Chake – Chake na Wilaya ya Mkoni.
*(b)* Kamati inashauri Tume kufanya bidii katika kutafuta usafiri wake wenyewe na kutotegemea magari ya kuazima kwa kazi za Tume.
*(c)* Kamati inashauri Tume wasitumie kipengele cha kuchukua fomu na kurejesha fomu kama chanzo cha Mapato ya Tume. hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Fedha inashauriwa kuacha kuitumia Tume kama chombo cha ukusanyaji wa mapato.

## 6.3 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

TASAF ni chombo muhimu ambacho kiliundwa kwa mashirikiano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kupambana na umasikini. Chombo hiki kinaendesha shughuli za usimamizi wa miradi kupitia ufadhili wa Washirika wa Maendeleo wakiwemo "World Bank, UNDP, DFID, UNICEF" pamoja na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Katika utekelezaji wa TASAF (III) Kamati imeridhishwa na mikakati na miradi inayotekelezwa kwa lengo la kupunguza umasikini kwa wananchi. Kwa upande wa Pemba Kamati ilifanikiwa kutembelea mradi mkubwa wa ujenzi wa Kituo cha afya, wodi ya wazazi na nyumba ya Daktari katika Shehia ya Kendwa, Wilaya ya Mkoani pamoja na mradi wa kujenga uzio na ukarabati wa Skuli ya Piki Wilaya ya Wete.

Aidha, Kamati imetembelea miradi inayotekelezwa kupitia Kaya Masikini na kupata kuzungumza nao kwa lengo la kutathmini mafanikio yanayopatikana kupitia miradi ya TASAF.

**Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu Kuu**

Mafanikio yafuatayo yamepatikana kutokana na utekelezaji wa programu hii:

*(a)* Kuimarika kwa hali za kiuchumi za walengwa kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini TASAF na kupungua malalamiko ya walengwa ambao walitolewa kimakosa katika mfumo wa malipo.
*(b)* Kubaini walengwa ambao walikuwa hawapati malipo kutokana na kutolewa kimakosa katika mfumo wakati wa uhakiki wa awali wa walengwa.
*(c)* kuwarudisha baadhi ya watu ambao walitolewa kwenye mfumo kimakosa.
*(d)* Kuwajengea vituo ya Afya vya kisasa wananchi ambavyo vinawasaidia kupata huduma bora.

### Changamoto za Utekelezaji wa Programu

Utekelezaji wa programu kuu hii unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

*(i)* Njia zinazotumika kupata walengwa wa kaya masikini zinachangamoto hivyo kupelekea baadhi ya wanajamii wenye mazingira magumu ya maisha kushindwa kuingizwa katika mfumo nakuwa wanufaika wa mradi huu.
*(ii)* Baadhi ya wanajamii hawatoi taarifa sahihi wanaposajiliwa au kuhakikiwa na hivyo kupelekea kuwepo kwa taarifa zisizosahihi, athari yake ni kutolewa katika mfumo au kupata fedha tofauti na matarajio.
*(iii)* Baadhi ya wanajamii hawatumii fedha kwa malengo yaliyokusudiwa bali huzitumia nje ya matarajio ya mradi na hivyo kuchelewa kufikia malengo ya kujikwamua kiuchumi.

### Maoni, Ushauri wa Kamati kwa TASAF

Katika utekelezaji wa mradi wa TASAF (III) Kamati inashauri mambo yafuatayo:

*(i)* Kwanza kabisa, Kamati inachukua fursa hii kuzipongeza Serikali zote mbili, Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi zao za kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kwa ufanisi. Aidha shukurani za pekee zimfikie Mkurugenzi Mkuu wa TASAF, Ndugu Mwamanga kwa jitahada zake za kufanikisha mradi huu bila upendeleo wowote.
*(ii)* Kamati pia, inatoa shukurani za dhati kwa watendaji wote wa TASAF pamoja na Makao Makuu yake kwa kuetekeleza vyema malengo ya mradi huu hapa Zanzibar. Utekelezaji wa miradi ya TASAF imeleta taaswira nzuri kwa jamii ya wazanzibari.
*(iii)* Uhakiki na usajili wa Kaya Masikini ufanyike kwa kuzingatia vigezo anuai ambavyo vimeainishwa kwa mujibu wa muongozo wa mradi.

*(iv)* Aidha, Kamati inaishauri Afisi ya Makamu wa Pili kufuatilia kwa ukaribu na kuweza kubaini kama fedha zinazopangwa Zanzibar kwa ajili ya mradi huu zinakidhi mahitaji na kufikia malengo yake kwa jamii au bado kuna mahitaji zaidi ambayo yanahitajika kwa ajili ya maboresho.

*(v)* Wasimamizi wa mradi wafuatilie moja kwa moja maendeleo ya miradi inayoanzishwa katika jamii na kutatua changamoto ndogo ndogo ambazo zinajitokeza katika miradi hiyo.

*(vi)* Kamati imeridhishwa na miradi yote ya afya iliyotekelezwa kwa kipindi hiki ambapo imeshakamilika kwa asilimia mia moja pamoja na ile miradi ya ujenzi na ukarabati wa skuli mbali mbali za Unguja na Pemba.

*(vii)* Kamati kwa upekee inashauri itakapofika kuanza kazi kwa kituo cha Afya cha Uzi ajira za wafanyakazi wa Kituo hicho kupitia vigezo vinavyohitajika waangalie zaidi wazawa wa kisiwa hicho.

## SEHEMU YA TATU

## MAONI, USHAURI WA JUMLA WA KAMATI NA HITIMSHO

Katika sehemu hii, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa itaeleza maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa Wizara tano zilizo chini ya Kamati hii.

## 7.0 MAONI NA USHAURI WA JUMLA

Kiujumla, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Taasisi zote ambazo zinasimamiwa na Kamati hii kutokana na juhudi zao kubwa wanazozichukua katika utekelezaji wa majukumu yao kufuata muongozo na taratibu za kisheria.

Hivyo, mbali ya maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa kwa kila Sekta na kila Taasisi, Kamati pia inatoa maoni, ushauri na maelekezo ya jumla kwa Taasisi hizo kama ifuatavyo:

### Ofisi ya Rais Ikulu

*(a)* Kamati inatoa pongezi za dhati kabisa kwa Ofisi hii kutokana na mafanikio mbali mbali yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti yake kwa mwaka 2022/2023 sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025. Aidha, Kamati imeridhishwa na namna Ofisi hii inavyozisimamia Taasisi za Umma katika kutekeleza maagizo ya Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Hussein Ali Mwinyi pamoja na viongozi wengine wakuu wa nchi.

*(b)* Kamati inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanya ukarabati Mkubwa wa Ikulu ya Dar es Salaam iliyopo mtaa wa leibon na Ikulu ya Dodoma. Hata hivyo, Kamati inashauri kujengewa uzio ikulu ya Dodoma pamoja na kufunga kamera za usalama.

*(c)* Kamati inaishauri Serikali kupitia Taasisi ya Nyaraka na Kumbumbu za Taifa kuzidisha mashirikiano na Taasisi za Umma na Binafsi kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu na kutunza historia ya Zanzibar. Aidha, Kamati inaishauri Taasisi hii kujenga mashirikiano ya karibu na Taasisi ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweka mifumo bora ya kielektroni katika kuhifadhi na kulinda Nyaraka kwa njia za kisasa.

*(d)* Kamati vile vile, inaishauri Serikali kuendeleza mpango wa ujenzi wa jengo jipya la Nyaraka katika eneo la Kilimani baada ya kukamilika kwa mpango wa manunuzi ya nyumba mbili zilizokaribu na ofisi hii.

*(e)* Aidha, Kamati inashauri mpango wa mradi unaoandaliwa wa ujenzi wa jengo jipya la Nyaraka kufanywa kwa haraka na kuwashirikisha wataalamu wa pande zote mbili za Muungano ili kupata ushauri wa kitaalamu wa masuala ya uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa kufuata utaratibu na miongozo ya nchi yetu.

*(f)* Kamati pia, inashauri kwa upande wa Pemba kutafuta eneo kubwa na lakutosha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi mpya ya Nyaraka.

*(g)* Kamati imesikitishwa na kuona zipo baadhi ya Taasisi ambazo hazitekelezi kwa vitendo Miongozo na mafunzo ya Utunzaji na Udhibiti wa Siri za Serikali yanayotolewa na GSO katika utendaji wao wa kazi wa kila siku. Hivyo, Kamati inazitaka taasisi husika kuwachukulia hatua watumishi wote wanaokaidi miongozo hiyo kwa vitendo.

**Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora**

(a) Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Ofisi hii kwa kusimamia vyema majukumu yake na kutoa miongozo kila inapostahiki juu ya masuala ya sheria na utumishi. Kamati inashauri Ofisi kufuatilia zaidi utendaji wa

Tume za Utumishi na kuzishauri kufuatilia na kusimamia watumishi wao katika kutoa huduma bora kwa jamii.

(b) Kwa upande mwengine, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Taasisi za Dini katika kujenga amani kwa waumini wa Dini zote pamoja na kuhakikisha amani na utulivu wa nchi yetu umelindwa kwa misingi ya Dini. Aidha, Kamati inaipongeza Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake na kuhakikisha migogoro ya Dini imepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na hatua mbali mbali zinazochukuliwa katika kukabiliana na changamoto za waumini. Hata hivyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar isichoke kuchukua hatua na kutoa miongozo ya kidini wakati wote wanapoona inafaa kufanya hivyo.

(c) Aidha, katika kujenga misingi bora ya Haki na mustakbali uliobora katika nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali kuzitumia Taasisi za kusimamia Haki Jinai kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na uwezo wake wa kuendesha kesi za udhalilishaji katika jamii na athari za kuacha kutumia sheria katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

(d) Kwa upande wa Sekta ya Utumishi wa Umma, Kamati inashauri kuchukuliwa hatua za haraka changamoto ya upotevu wa Majalada au baadhi ya taarifa muhimu kwa baadhi ya wastaafu waliotumikia utumishi wao zaidi ya Taasisi moja katika Serikali na kukosekana kwa baadhi ya vielelezo muhimu katika majalada ya wastaafu mfano; mikataba, aridhilhali, barua za vizuizi vya mishahara vithibitisho vya kifo, barua za bodi ya madaktari nakadhalika.

(e) Aidha, Kamati inasikitishwa na kitendo cha ujazaji usioridhisha wa taarifa za mishahara katika kalamazuu na kupelekea kukosekana kwa usahihi wa taarifa za hesabu za mafao kwa baadhi ya wastaafu. Kamati inashauri taasisi inayohusika kufanya ukaguzi wa suala hili kufuatilia kwa kina kuona chanzo cha changamoto hii ili taasisi zitakazobainika kuchukuliwa hatua za msaada.

(f) Kamati ilipata kutembelea na kukagua eneo lenye kiwanja cha Chuo cha Utawala wa Umma kwa upande wa Pemba na kuona changamoto zilizomo katika eneo hili. Kamati haikuridhishwa na eneo hili kwa ujenzi wa Chuo na hivyo, inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuzuia ujenzi ambao umepangwa kufanywa katika eneo hili na hivyo kutafuta eneo jengine ambalo litakuwa rafiki katika mazingira ya Chuo lakini pia halitaigharimu Serikali fedha nyingi

kwa ajili ya ujenzi.

**Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ**

*(a)* Kamati inaishauri Serikali kuziagiza Mamlaka zinazohusika na kutoa mgawanyo wa fedha za maliasili na kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa fedha hizo kwa wakati.
*(b)* Serikali izisaidie Halmashauri zote kuanzisha mradi wa kuzalisha umeme wa gesi asilia na mbolea kama nishati mbadala katika kutunza mazingira kwa kuepusha kutumia kuni ambazo zinapelekea ukatwaji wa miti kwa kiwango kikubwa katika misitu iliyotuzunguka.
*(c)* Kamati inashauri Wizara kuaandaa programu maalumu ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo katika kuendeleza na kukuza biashara zao kwenye kila Halmashauri za Unguja na Pemba.
*(d)* Katika ujenzi wa miradi ya masoko ya wajasiriamali kwa kila Wilaya; Kamati inashauri Wizara kuzisimamia Serikali za Mikoa na kuhakikisha maeneo hayo wanapewa wafanyabiashara waliokusudiwa ili kuepusha maeneo hayo kumilikiwa na watu wasiokuwa walengwa.
*(e)* Kamati inashauri Serikali kuzisimamia Mamlaka husika katika utoaji wa leseni za biashara za vileo kuweka utaratibu wa wazi na shirikishi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ukusanyaji na utaratibu wa Matumizi.
*(f)* Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhakikisha kuwa wapiganaji na watendaji wote wa Vikosi vya SMZ wanalipwa stahiki zao za likizo pamoja na fedha za muda wa ziada (over time).
*(g)* Kamati inashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wamezidisha nguvu ya kufanya usafi na ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri zao zote za Unguja na Pemba.
*(h)* Aidha, Kamati haikuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa vyoo vya skuli ya Uchukuni na hivyo, inaliagiza Baraza la Mji Kati kuhakikisha ujenzi huu unakamilishwa kwa wakati na kumsimamia mkandarasi kutimiza makubaliano ya mkataba.
*(i)* Vile vile kamati inaitaka Wizara kuingilia kati mgogoro wa kiuendeshaji baina ya madiwani na Mkurugenzi wa Baraza la Mji Kati.
*(j)* Sambamba na hilo, kamati inaitaka Wizara kumaliza mgogoro wa Baraza la Mji Kaskazini B kwa upande mmoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa kaskazini unguja kwa Upande mwengine. pamoja na kulifanyia haraka suala la kupatika Mwenyekiti wa Baraza hilo lla kaskazi B ambae aliondolewa na vikao halali kwa zaidi ya miezi sita iliyopita.
*(k)* Kamati kufuatia malalamiko ya Manispaa ya Magharibi A kuhusu kuzuiliwa kwa Mnada Inashauri kila Halmashauri iweze kuruhusiwa

kufanya Mnada wake ili kutoa huduma za karibu kwa wananchi ili kuongeza mapato na maslahi ya halmashauri hizo.

*(l)* Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mradi wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vya Idara Maalum ili kuweka mazingira bora ya kujifunzia.

*(m)* Kamati pia, inaishauri Serikali kuunganisha nguvu za Idara Maalum katika kupiga vita matukio ya kihalifu katika jamii.

*(n)* Sambamba na hayo, Kamati pia inaishauri Serikali kuweka fungu maalum la mafuta kwa vyombo vya KMKM na Zimamoto katika kuendeleza doria za baharini na misingi ya kazi zao halisi ili kuzuia na kupambana na matukio ya kihalifu.

*(o)* Kamati inaitaka Wizara kueleza hatma ya ujenzi ya kampuni ya Ujenzi ambayo imekua ikionekana kukosa kazi kwa sasa na badala yake kazi hiyo kuchukuliwa na vikosi vyenyewe.

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

(a) Kwa ujumla, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais kwa kutekeleza vyema majukumu yao na kuhakikisha Sera na Miongozo ya Serikali imetekelezwa ipasavyo ili kuifikisha nchi yetu katika maendeleo.

(b) Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika biashara ya Kaboni ambayo inachukua nafasi kubwa katika kuhifadhi mazingira. Jamii pia ishajihishwe kutumia nishati mbadala ya matumizi ya majumbani na kupanda miti kwa wingi kama ni njia mbadala ya kukabiliana na janga la mabadiliko ya tabianchi.

(c) Sambamba na hayo, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuvuka malengo katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na ada ya uhifadhi na ukaguzi wa Mazingira kwa upande wa Unguja, ambapo katika kipindi cha July – Septemba 2022 walifikia asilimia 112%. Aidha, Kamati inashauri mafanikio haya pia yasimamiwe kwa upande wa Pemba ili kwenda sambamba na malengo ya Mamlaka katika ukusanyaji wa mapato.

(d) Kamati pia, inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kutekeleza vyema miradi ya uhifadhi wa mazingira katika maeneo ya Tovuni Wilaya ya Wete, Sipwese Wilaya ya Mkoani na Likoni katika Wilaya ya Wete. Vile vile, Kamati ilipata fursa ya kufika Mkoni Mtwara katika fukwe ya Mikindani na kuona namna miradi kama hii inavyotekelezwa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kamati inashauri miradi kama hii pia ifanywe katika fukwe ya Kichanjaani katika Shehia ya Ndagoni Wilaya ya Chake – Chake kutokana na athari kubwa za

kimazingira zinazoendelea kutokea.

(e) Wizara itumie nguvu kubwa ya kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuwatunza na kuwalinda waathirika wa dawa za kulevya wakati wanapoacha kutumia dawa na kuwa wananchi wema katika jamii.Pamoja na hilo. Kamati inaitaka Serikali kutafuta uwezekano wa kujenga nyumba ya waraibu wa dawa za kulevya iliyo salama na kuachana na nyumba za kukodi ambazo zipo katikati ya makaazi ya watu kisiwani Pemba.
(f) Kamati pia, inaishauri Serikali kuongeza programu za kutoa elimu ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza ikiwemo virusi vya HIV na UKIMWI, sambamba na hilo, kamati inashauri kuongeza bajeti ya Tume hiyo ili kuepuka kufanya kazi kwa kutegemea wafadhili.
(g) Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa kumteuwa Ndugu Ussi Khamis Debe kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Watu wenye Ulemavu. Aidha, Kamati inaipongeza Ofisi kwa kusimamia vyema programu ya Watu wenye Ulemavu na kuhakikisha wametekeleza majukumu yao kwa uweledi na ufanisi katika kuwahudumia watu wenye Ulemavu. Aidha, Kamati imepata faraja sana kuona Idara hii imepata Sheria mpya ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa) ambayo imeweka wazi haki na fursa za Watu wenye Ulemavu katika jamii.
(h) Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kuipatia msaada Idara ya Watu wenye Ulemavu Pemba kwa kuwajengea Ofisi yenye nafasi na kuwapatia vifaa na mazingira bora ambayo yatawezesha kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na kupata maslahi yatakayosaidia kujenga maisha yao.

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi**

*(a)* Kamati inashauri wizara kufuatilia na kusimamia kikamilifu taasisi za umma katika kutoa huduma zilizobora na kuhakikisha kuwa miongozo na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa ipasavyo.
*(b)* Kamati inaishauri Serikali kuzidisha kasi ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya TASAF III ya ajira za muda mfupi na zenye tija ambazo zinaibuliwa na wananchi ambapo jumla ya Shehia 126 za mpango wa awali zimenufaika.

*(c)* Kamati pia, imeridhishwa na utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya ujenzi wa kituo cha afya daraja la II (PHC+) katika Shehia ya Uzi na ujenzi wa jengo la wazazi na kituo cha afya Vijibweni katika Shehia ya Donge Pwani ambapo kwa pamoja miradi hii ujenzi wake imeshafikia wastani

wa asilimia 70.

*(d)* Aidha, Kamati inashauri kwa ile miradi mipya ambayo imepangwa kutekelezwa kwa mwaka huu na bado haijaanza, ni vyema Wizara kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa wakati na kwa manufaa mapana ya wananchi.

*(e)* Kamati inashauri Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na wizara hii kuzidisha kasi ya kusimamia na kufuatilia haki na fursa za watendaji wa Baraza katika nyanja zote za kimaslahi na mafunzo ili kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi.

*(f)* Vile vile, Kamati inashauri Afisi ya Baraza la Wawakilishi kuandaa mradi maalumu wa ujenzi wa jengo jipya la ofisi na kumbi za Kamati pamoja na gari kwa ajili ya matumizi ya Baraza hasa Kamati za Kudumu na kuwasilisha maombi Serikalini kwa haraka ili mradi huu upate kuombewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake.

*(g)* Katika maboresho ya Afisi ya Pemba, Kamati inashauri kusimamia kikamilifu matengenezo ya Ukumbi mkubwa wa mikutano pamoja na ofisi zake ili kuweka mazingira bora ya utendaji na shughuli zote za Serikali zinazofanyika hapo.

*(h)* Aidha, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Afisi ya Baraza Pemba kutokana na juhudi zao za kutoa huduma kwa waheshimiwa wajumbe pamoja kutekeleza vyema majukumu yao ya kila siku.

*(i)* Sambamba na hayo, Kamati inashauri Afisi ya Baraza izidishe kasi ya kutoa mafunzo kwa watendaji wake ili kupata watendaji wenye uzoefu na wanaoendana na wakati na mazingira ya mabunge.

## 8.0 HITIMISHO

Katika kukamilisha kazi hii, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa haina budi kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kusimamia vyema sera na mipango ya Serikali katika utekelezaji wa shughuli zake za kuwaletea wananchi maendeleo ambao ni msingi mkuu wa utawala wake.

Kwa upande mwengine, Kamati inatoa shukurani zake za dhati kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ndugu Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati pamoja na wanasheria wetu wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa msaada wao mkubwa ambao wamekuwa wakiipatia Kamati hii wakati wa upitiaji wa Miswada ya Kisheria.

Aidha, pongezi maalum ziende kwa upande wa uongozi na watendaji wote

wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba, watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; watendaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; na watendaji wa Afisi ya Rais Ikulu pamoja na Afisi kuu ya Baraza la Wawakilishi Unguja kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii, katika kipindi chote ambacho Kamati ilitekeleza majukumu yake na inawaomba waendelee kutoa ushirikiano na msaada wao wa dhati kila itakapohitajika.